

ATHARI YA KIMAKUNDUCHI KATIKA KISWAHILI SANIFU

RUKIA RAMADHAN BUNDA LLA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI
YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasnifu hii iitwayo “ **Athari ya Kimakunduchi Katika Kiswahili Sanifu**” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

.....
Dkt. Nestory N. Ligembe

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhisiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe yote au sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila ya kibali cha maandishi ya Mkuu wa Kurugenzi ya Elimu za Uzamili kwa niaba ya mwandishi na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, Rukia Bundalla, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyingine yoyote.

.....

Sahihi

.....

Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa baba yangu mzazi Ramadhan Bundalla Ramadhan kwa malezi yake mazuri na kwa kunipatia msingi wa elimu yangu. Hakika upendo wake wa dhati ulikuwa nguzo tegemewa kwa maisha yangu bila yeye nisingefika hapa. Hakika nitamuenzi daima. Pia, kazi hii naitabaruku kwa mume wangu mpenzi Abdalla Omar Abdalla na watoto wangu Omar na Aboubakar kwa uvumilivu na kujinyima mengi kwa kipindi chote nilichokuwa masomoni.

SHUKRANI

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na nguvu kwa kipindi chote cha masomo yangu mpaka kufikia tamati katika kazi hii. Kazi ya utafiti sio rahisi; inahitaji ushirikiano. Ndiyo maana wahenga walisema, *kidole kimoja hakivunji chawa*. Hivyo utafiti huu umetokana na michango na mawazo ya watu mbalimbali ambao sitawataja wote kutokana na wingi wao na ufinyu wa nafasi bali nachukua fursa hii kuwashukuru wote.

Shukrani za pekee kutoka moyoni zimwendee mwalimu na msimamizi wangu, Dr Nestory N. Ligembe, kwa msaada wake mkubwa na maelekezo yake ya kitaaluma aliyonipatia katika kipindi chote cha utafiti. Alijitolea muda wake na kuwa tayari kuisoma kazi yangu, kuirekebisha, kunipa maelekezo na kunishauri kila ilipobidi bila kuchoka licha ya kuwa na majukumu mengi. Maoni na maelekezo yake ndio yaliyofanikisha kazi hii. Namwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe baraka na maisha marefu.

Namshukuru Mkuu wa Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu na wahadhiri wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mafunzo yao mazuri waliyonipatia katika kiwango hiki cha umahiri.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu wa M.A Kiswahili mwaka 2015/2016 kwa ushirikiano na ushauri wa kitaaluma walionipatia kwa kipindi chote tulichokaa pamoja. Hali kadhalika nawashukuru wenyeji wote wa Makunduchi walionisaidia kunipa taarifa mbalimbali zinazohusu lahaja ya Kimakunduchi.

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo na majadwali. Sampuli iliyotumika ni sampuli nasibu rahisi. Eneo la utafiti ni Mkoa wa Kusini Unguja. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni dodoso, usaili pamoja na mahojiano. Utafiti huu umebaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wa Kimakunduchi, wanatumia makundi ya kijamii yanayotumia vipengele vya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu ni pamoja na wazee, vijana, walimu na wanafunzi. Sababu za kutumia vipengele hivyo zinatokana na kuathiriwa na lugha ya kwanza. Utafiti ulihitimisha kuwa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ni lahaja zinazotumika katika mawasiliano kwa wakaazi wa visiwa vya Unguja. Imebainika kuwa kuna misamiati inayofanana na misamiati inayotafautiana ambayo huleta vikwazo katika mawasiliano katika makundi hayo mawili. Mwisho utafiti huu unapendekeza watafiti wengine kufanya utafiti zaidi katika maeneo ya kimuundo, kimsamiati pamoja na athari za matamshi ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kuingizwa katika shughuli rasmi.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU.....	v
SHUKRANI.....	vi
IKISIRI	vii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xii
KIELELEZO	xiv
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Tatizo	1
1.3 Tatizo la Utafiti	4
1.4 Malengo ya Utafiti	4
1.4.1 Lengo Kuu.....	5
1.4.2 Malengo Mahususi	5
1.5 Maswali ya Utafiti.....	5
1.5.1 Umuhimu wa Utafiti.....	5
1.6 Mipaka ya Utafiti	7
1.7 Maadili ya Utafiti	7
1.8 Vikwazo vya Utafiti	8
1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti.....	8
1.10 Hitimisho.....	9

SURA YA PILI.....	10
2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI.....	10
2.1 Utangulizi.....	10
2.2 Dhana ya Lahaja ya Kimakunduchi.....	10
2.3 Kiswahili Sanifu na Usanifishaji Wake.....	13
2.4 Tofauti ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.....	17
2.4.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti wa Kisayansi.....	18
2.4.2 Mkabala wa Kinadharia.....	21
SURA YA TATU.....	27
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....	27
3.1 Utangulizi.....	27
3.2 Mkabala wa Utafiti.....	27
3.3 Muundo wa Utafiti.....	28
3.4 Mbinu za Utafiti.....	28
3.4.1 Mbinu ya Usaili.....	28
3.4.2 Mbinu ya Hojaji.....	29
3.5 Mbinu ya Ushuhudiaji.....	30
3.6 Eneo la Utafiti.....	30
3.7 Sampuli na Usamplishaji.....	31
3.8 Zana za Utafiti.....	32
3.9 Mbinu za Kukusanyia Data.....	33
3.9.1 Data za Upili.....	33
3.9.2 Data za Msingi.....	34
3.10 Uchambuzi wa Data.....	34

3.11	Hitimisho	35
SURA YA NNE.....		36
4.0	UWASILISHAJI MATOKEO NA MAJADILIANO	36
4.1	Utangulizi	36
4.2	Taarifa za Kiisimujamii za Watafitiwa	36
4.2.1	Matumizi ya Kimakunduchi Kwa Jamii ya Wamakunduchi.....	37
4.3	Kubainisha Msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu .	38
4.4	Msamiati wa Kazi Mbali Mbali	41
4.5	Misamiati ya Nambari za Msingi	41
4.6	Msamiati wa walemavu.....	42
4.7	Msamiati ya Majina ya Ukoo	43
4.8	Msamiati ya Mapambo, Mila na Utamaduni.....	44
4.9	Msamiati ya Nyakati	44
4.10	Msamiati ya Malipo	45
4.11	Athari Za Lahaja Ya Kimakunduchi	47
4.12	Udondoshaji wa Nazali katika Msamiati	49
4.13	Udondoshaji wa Kilainisho/ l/ na Kimadende / r/.....	50
4.14	Uingizaji wa Sauti -y-, pamoja na Uingizaji wa Sauti kuwa -lya-	51
4.15	Uingizaji wa Sauti/ nch /,k/,j / ,/w /.....	52
4.16	Uingizaji wa Sauti /v/ na / vy /katika Lahaja ya Kimakunduchi.....	53
Jadweli Na 4.17: Uingizaji wa sauti /v/ na /vy/.		54
4.17	Athari za Kiumbo	55
4.18	Matamshi ya Kimakunduchi Yanavyoathiri Kiswahili Sanifu	57
4.19	Matamshi Ya Kimakunduchi Yenye Uvokali/ o, e, u, i, a /	60

4.20	Matamshi Kubadilika umbo	62
4.20.1	Tofauti Katika Matamshi ya Mazungumzo ya kawaida.....	63
4.20.2	Matamshi ya Sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho /l/.....	65
4.21	Kuwekwa Vipindi Maalum Katika Vyombo Vya Habari	75
4.22	Lahaja Itumike Mashuleni.....	76
4.23	Kuwekwa Kwa Tamasha La Utamaduni Asilia	76
4.24	Kutoruhusu Kuingia Kwa Wageni Kiholela	77
4.25	Kutumika Kwa Sarufi Moja	77
4.26	Kuwepo Kwa Kumbukumbu Za Kutosha	78
4.27	Muhtasari wa Sura ya Nne	78
	SURA YA TANO	80
	5.0 MUHTASARI NA MAPENDEKEZO	80
5.1	Utangulizi	80
5.2	Muhutajari kuhusu Utafiti.....	80
5.3	Matokeo ya Utafiti	82
5.2.1	Mapendekezo Kuhusu Utafiti Zaidi	85
	MAREJEO.....	86
	VIAMBATANISHO.....	88

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 1.1:	Tofauti Baina ya Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu	3
Jedwali Na 2.1:	Kufanana kwa Misamiati ya Lahaja za Wahamiaji na Lahaja ya Kimakunduchi	12
Jedwali Na 2.2:	Tofauti Baina ya Lahaja Ya Kimakunduchi Na Kiswahili Sanifu.....	18
Jedwali Na 3.1:	Sampuli ya Watafitiwa Katika Maeneo Teule ya Makunduchi ..	32
Jedwali Na 4.1:	Taarifa za Kiisimujamii za Watafitiwa	37
Jedwali Na 4.2:	Uzungumzaji wa Kimakunduchi Shuleni.....	38
Jadweli Na 4.3:	Misamiati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu	55
Jadweli Na 4.4:	Misamiati wa Kazi Mbalimbali	41
Jadweli Na 4.5:	Misamiati wa Nambari za Msingi	42
Jadweli Na 4.6:	Misamiati wa Walemavu	42
Jadweli Na 4.7:	Misamiati ya Majina ya Ukoo	43
Jadweli Na 4.8:	Misamiati ya Mapambo, Mila na Utamaduni.....	44
Jadweli Na 4.9:	Misamiati Ya Nyakati.....	45
Jadweli Na 4.10:	Misamiati Ya Masaa Ya Siku.....	45
Jadweli Na 4.11:	Misamiati ya Malipo ya Kifedha.....	46
Jadweli Na 4.12:	Athari za lahaja ya Kimakunduchi	47
Jadweli Na 4.13:	Udondoshaji wa Nazali Katika Misamiati.....	49
Jadweli Na 4.14:	Udondoshaji wa Kilainisho /l / na Kimadende / r/.....	50
Jadweli Na 4.15:	Uingizaji wa sauti-y-,na kuwa -lya-	51
Jadweli Na 4.16:	Uingizaji wa Sauti /nch/, / k/ na /w/	53

Jadwali Na 4.17:	Uingizaji wa sauti /v/ na /vy/.....	54
Jadwali Na 4.18:	Athari za Kiumbo	55
Jadwali Na 4.19:	Athari katika Matumuzi ya Lahaja ya Kimakunduchi	56
Jedwali Na 4.20:	Konsonanti na Nusu Irabu za Kimakunduchi.....	59
Jedwali Na 4.21:	Kubadilika umbo katika Matamshi	62
Jedwali Na 4.22:	Tofauti katika Matamshi ya Mazungumzo ya Kawaida.....	64
Jedwali Na 4.23:	Matamshi ya Sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho /l/...	65
Jedwali Na 4.24:	Matamshi ya Sauti /kana/ badala ya /ana/:	67
Jedwali Na 25:	Matamshi ya Sauti /cha/ badala ya /ta/	68
Jedwali Na 4.26:	Misamiati Inayowiana Baina ya Kiswahili Sanifu na Lahaja ya Kimakunduchi	69
Jedwali Na 4.27:	Kubainisha Msamiati Inayotokana na Lahaja ya Kimakunduchi	71
Jedwali Na4.28:	Kubainisha Utamkaji wa Asili na Utamkaji Wa Sasa.....	72
Jedwali Na 4.29:	Maoni Juu ya Kupunguza Athari za Kimakunduchi Katika Kiswahili Sanifu	74

KIELELEZO

Kielelezo Na 4.1: Eneo Ambalo Sauti Zenye Uvokali Hutolewa 61

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulihusu athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Lengo kuu ni kuchunguza athari za lahaja Kimakunduchi katika lugha ya Kiswahili sanifu. Sura hii imegawanywa katika sehemu tisa. Sehemu ya kwanza, inaelezea usuli wa tatizo la utafiti. Sehemu ya pili, ilielezea tatizo la utafiti. Sehemu ya tatu, ilielezea malengo ya jumla na malengo mahususi. Sehemu ya nne inahusu maswali ya utafiti. Sehemu ya tano, ilionesha umuhimu wa utafiti. Sehemu ya sita, inafafanua mipaka ya utafiti. Sehemu ya saba, imeelekeza maadili ya utafiti. Sehemu ya nane, ilieleza juu ya vikwazo vya utafiti. Sehemu ya tisa ni muhtasari wa sura ya kwanza.

1.2 Usuli wa Tatizo

Lahaja katika lugha ya Kiswahili kuna tofauti mbalimbali zinazojitokeza kutoka lahaja moja na nyingine. Miongoni mwa mambo yanayotofautisha lahaja hizo ni lafudhi, fonolojia na msamiati Masebo na Nyangwine (2006:2007:2008).

Lahaja ni tofauti ndogondogo zinazojitokeza katika lugha kuu yenye asili moja. Tofauti hizo ziko katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno Kipacha (2003). Utafiti huu umejikita zaidi katika lahaja ya Kimakunduchi kwa kuchunguza athari za mawasiliano zinavyokwamiza kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Kimakunduchi ni lahaja inayojulikana kwa majina mbalimbali kama vile Kikae, Kikale au Kihadimu, huzungumzwa

sehemu za Kusini Mashariki ya visiwa vya Uzi. Kimakunduchi ni lahaja inayozungumzwa katika mji wa Makunduchi na viunga vyake Juma (2011). Kwa hivyo kimantiki asili ya jina Makunduchi itapatikana kwa kuchunguza asili ya jina Makunduchi, huko Kae pwani, baadhi yao waliondoka kuelekea kusini Mashariki kupitia sehemu mbalimbali na kufikia sehemu yenye udongo mwekundu. Hapa kundi hili lilisita na kuanza shughuli za kilimo, baada ya muda Fulani wengine walirudi kule Kae na walipoulizwa na wenzao walikuwa wapi? Wakajibu.

Tuwa ukonyikunduchi, kwa maana walikuwa wakiishi mahali ambako ardhi yake ni nyekundu, kwa kuwa hawakuweza kulipata jina hasa la mahali penyewe, hivyo tamko nyikundu chi wakatia wepesi zaidi. Kwa hiyo taratibu jina hili likaanza kufanyiwa mabadiliko madogo madogo na hatimae likapatikana jina la Makunduchi na lugha ya watu hawa ikaitwa Kimakunduchi.

Kimakunduchi kina msamiati wa asili ya lugha za Kibantu ukilinganisha na Kiswahili sanifu ambacho kimeathiriwa na mwingiliano wa watu unaotakana na biashara au utawala, jambo ambalo limesababisha kuingia kwa msamiati mwingi wa Kiarabu na Kiingereza.

Lahaja ya Kimakunduchi ni lahaja inayozungumzwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya Kusini Unguja. Watumiaji wa Kimakunduchi wa maeneo hayo wanatofautiana katika kiimbo, sauti, mkazo na msamiati. BAKIZA (2012). Aidha tahajia ya lahaja ya Kimakunduchi yaani uwakilishi wa herufi zinazounda neno

katika maandishi wanatofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Baadhi ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi hutofautiana na Kiswahili sanifu. Kwa mfano:

Jedwali Na 1.1: Tofauti Baina ya Msamiati wa Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
<i>Sh</i> ingo	<i>Si</i> -ngo
<i>Ji</i> cho	<i>Di</i> -cho
<i>Ji</i> no	<i>Gi</i> –no

Chanzo: BAKIZA, 2012

Katika jedwali 1.01 linaonesha tofauti za kimatamshi baina ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika msamiati iliyopo katika jedwali hilo.

Tofauti za kimatamshi, msamiati na lafudhi kati ya lahaja moja na nyengine. Kama inavyoonekana katika jedwali neno shingo hutamkwa singo katika Kimakunduchi, neno jicho hutamkwa dicho katika Kimakunduchi, na neno jino katika Kiswahili Sanifu na kwa lahaja ya Kimakunduchi hutamkwa gino, kwa hiyo ni wazi hutofautika katika matamshi, kama jedwali linavyoelezwa na kuthibitika kwa athari mbalimbali zikiwemo za kimatamshi za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu Masebo na Nyangwine (2006: 2007: 2008).

Uteuzi wa Kiswahili sanifu ilikuwa ni historia ya mchakato wa usanifishaji wa Kiswahili iligubikwa na malumbano juu ya launi ipi iwe ya msingi kati ya Kiamu, Kimvita na Kiunguja, ambako ilikubalika kwa sauti moja ya kuteua Kiunguja kuwa ndio msingi wa Kiswahili Sanifu katika kilichofanyika mjini Mombasa mnamo mwaka (1928) na kufuatiwa na uundwaji wa kamati ya

Kiswahili sanifu ya Afrika Mashariki KKAM mwezi Januari mwaka (1930) ndipo kilipoamulika kutumika katika shughuli rasmi kama vile, elimu, biashara, dini, siasa, vyombo vya habari na shughuli nyingine zinazotumika ndani ya jamii. huenda vimechangia kuwepo kwa matumizi mbalimbali ya matamshi, miundo ya msamiati na mawasiliano baina ya wazungumzaji Wikipedia (2014).

Kwa maelezo haya ,utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu na jinsi zinazokwamisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa makundi hayo mawili.

1.3 Tatizo la Utafiti

Haja ya kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu ya Mapitio tofauti yaliyofanywa na mtafiti. Kwa mfano utafiti wa Juma,A (2011) katika tasnifu yake Ulinganishaji wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kizimkazi, Chuo Kikuu Cha Daresalam, katika tasnifu hii alitafiti mlingano wa kimakunduchi na lugha nyengine za Kusini.

Kwa hiyo mtafiti aliamua kufanya utafiti huu ulijikita kuchunguza athari za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu ambapo hazijachunguzwa na kuchambuliwa ili kubaini iwapo lahaja hio imeathiri Kimakunduchi au la, kwa kuzingatia matamshi ya wazungumzaji hao.

1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

1.4.1 Lengo Kuu

Utafiti huu unakusudia kuchunguza athari ya lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

1.4.2 Malengo Mahususi

- i) Kubainisha msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.
- ii) Kufafanua athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.
- iii) Kueleza tofauti baina ya msamiati unaowiana baina ya lahaja ya Kimakunduchi na ile ya Kiswahili sanifu.
- iv) Kueleza maoni ya watafitiwa jinsi ya kupunguza athari za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu.

1.5 Maswali ya Utafiti

- i) Je, kuna msamiati gani ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu?
- ii) Misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi inaathirije lugha ya Kiswahili Sanifu?
- iii) Kuna tofauti gani baina ya misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi na ile ya Kiswahili Sanifu?
- iv) Je, kuna haja ya kupunguza athari za Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu?
Toa maoni yako?

1.5.1 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umechunguza athari katika lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu utakuwa na umuhimu kama ifuatavyo:

Kwa wanataaluma: Utafiti huu umewasaidia wasomi wa vyuo vikuu kupata marejeleo ,pamoja na wahadhiri utawasaidia kuandaa mihadhara kwa wanafunzi wao kuhusiana na lahaja.Na wanaofanya utafiti utawasaidia kufanya mapitio ya tasnifu zao.

Kwa watunga sera: Utafiti huu utawasaidia watunga sera kutathmini juu ya umuhimu wa lahaja kwa kuonesha vipengele vya matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi vinavyotumiwa katika Kiswahili sanifu katika ukuaji na ueneaji katika jamii.Pia itasaidia kuona lahaja sanifu imefanikisha mawasiliano ya namna moja.

Kwa serikali: Utafiti huu utatoa mchango wa maarifa katika nyanja za kiserikali kuwa ni lazima kutumia katika shughuli za kitaifa na kusaidia kutangaza utamaduni hasa kwa kuangalia lahaja zilizomo Tanzania.Kiswahili ni lugha ya Taifa katika nchi za Afrika Mashariki na hadi kuwa lugha ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwa miongoni mwa lugha rasmi za Umoja wa Afrika.

Kwa Watanzania: Utafiti umewasaidia Watanzania kufahamu lahaja na kumtambulisha mzungumzaji wa jamii ya Wamakunduchi na mahali anakotoka.Hivyo ni vigumu kumtenganisha mwanadamu na lugha yake.

Kwa watafiti wengine: Utafiti huu umewasaidia kupata muongozo wa uchunguzi juu ya athari ya lahaja ya Kimakunduchi na ile ya Kiswahili sanifu kwenye

matamshi, misamiati inayotumika katika mawasiliano. Pia kutumia kama sehemu ya kazi tangulizi katika kukamilisha tasnifu zao.

Kwa taaluma ya isimu: Kwa wanaisimu utafiti huu umerejelewa katika kazi zao za kiisimu na huchota maarifa mapya ambayo yatayoonekana katika lahaja sanifu na lahaja ya Kimakunduchi na kupatikana athari ambazo huweza kuongeza msamiati mpya katika Kiswahili sanifu. Baadhi ya misamiati ya lahaja ya Kimakunduchi inayotumika sambamba na Kiswahili sanifu huweza kusanifiwa na kuwa katika lugha rasmi.

Kwa walimu na wanafunzi: Utafiti huu umewasaidia kupata marejeo yanayohusiana na athari za Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu na kuangalia mahusiano yaliyopo baina ya athari za lahaja za Kimakunduchi katika lugha ya Kiswahili Sanifu na jinsi athari hizo zinavyokwamisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja husika. Mtafiti alichunguza zaidi matamshi na kujikita katika kuchunguza athari nyengine za lahaja hii katika Kiswahili sanifu.

1.7 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alizingatia maadili ya kiutafiti na kuwa muwazi kwa walengwa, kuwasilisha data na matokeo kwa usahihi na uaminifu na kuzingatia malengo

mahususi. Aidha taarifa zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa zilitumika katika utafiti tu. Mtafiti aliweka wazi taarifa za watafitiwa bila ya kutaja majina yao kwa lengo la kuwalinda. Mtafiti alizingatia maswali ya kuuliza, muda wa kumaliza, faida na umuhimu wa utafiti. Pamoja na yote mtafiti aliepukana na kosa la kunakili kazi za watu, na kujielimisha kufuata sheria za nchi katika kufanya utafiti. Ni muhimu kuwa mnyenyekevu na wala usivunje mila na kanuni za utamaduni wa wahusika.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vya utafiti huu ambavyo mtafiti alikumbana navyo ni ugeni wa kijiji husika, hali ya hewa (miongo /msimu) ina maana ilikuwa siku za mvua usumbufu kwa walengwa kuwapata baadhi yao walikwenda katika shughuli za kilimo. Vilevile baadhi ya walengwa kutokuwa na utayari wa kujibu maswali na baadhi ya dodoso kutorejeshwa.

1.9 Utatuzi wa Vikwazo vya Utafiti

Vikwazo vya utafiti huu nilivitatua kwa kutafuta mwenyeji wa Makunduchi ambaye ni mahiri katika lahaja ya Kimakunduchi na ni muelewa wa kutosha wa utamaduni kwa eneo hilo.

Kwa upande wa hali ya hewa nilingalia msimu ambao wanakijiji hawafanyi Shughuli za kilimo na kuweza kuwapata wahusika katika makaazi yao.

Vile vile mtafiti alijaribu kutoa taaluma ya kutosha juu ya umuhimu wa utafiti huo kwa watafitiwa ambao waliokuwa hawana utayari wa kujibu maswali ya

utafiti. Pia niliwapa maelekezo ya kujaza dodoso na kuwasimamia na kuhakikisha dodoso zinajazwa vizuri.

1.10 Hitimisho

Sura hii ya utangulizi ambayo ilijengwa na vipengele tofauti, ambavyo ni usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, na kuelezea umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliweka mapitio kadhaa aliyoyapitia kabla ya kuihalalisha mada yake kwa kigezo cha kuchunguza iwapo iliwahi kutafitiwa au haijatafitiwa. Kutokana na baadhi ya mapitio aliyoyasoma mtafiti hayakufikia utafiti huo. Aligundua kuwa wapo watafiti walioitafiti lahaja ya Kimakunduchi, lakini hawakuelekea katika mwelekeo wa utafiti huu. Lengo la mapitio ni kufahamu mapengo ambayo hayajafanyiwa uchunguzi, hivyo kufanya utafiti ili kuziba pengo hilo. Sura hii imegawanywa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza, ilihusu dhana ya lahaja ya Kimakunduchi. Sehemu ya pili ilihusu Kiswahili sanifu na usanifishaji wake. Sehemu ya tatu ilihusu tofauti ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi. Sehemu ya nne ilihusu, mapitio ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

2.2 Dhana ya Lahaja ya Kimakunduchi

Lahaja ni lugha moja wapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa ni lugha moja isipokuwa zinazotafautiana katika lafudhi au msamiati usiokuwa wa msingi Massamba (2004). Watumiaji wa lahaja ya Kimakunduchi hutumia msamiati tofauti katika mawasiliano. Katika Kiswahili kuna lahaja (15).

Lahaja hizo zimeenea katika eneo la Afrika Mashariki na tabia zinazoonisha kuwa zote zina msingi mmoja wa lugha ya Kiswahili ambayo ina asili ya

Kibantu.Lahaja ambazo ziko katika ukanda wa pwani katika visiwa vya Zanzibar ni Kiunguja,Kitumbatu,Kihadimu(Kimakunduchi) na Kipemba.Na katika utafiti huu tutaanagili lahaja ya Kimakunduchi.

BAKIZA(2012) linafafanua Lahaja ya Kimakunduchi ni lahaja inayozungumzwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya Kusini Unguja.

Sehemu kubwa ya Kusini hutumia Kikae,(Kimakunduchi) katika mkoa wa kusini,hasa wilaya ya Kusini Unguja,kuna miji kama vile Pete, Jambiani, Muungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni, Mtende, na Makunduchi yenyewe ambayo ndio makao makuu ya lahaja ya Kikae . Kwa vile ni lugha inayozungumzwa na kikundi kidogo tu cha watu lugha hizi zinakuwa na sifa zifuatazo:

*Huzungumzwa na watu au kikundi maalumu na mahala maalumu:*Yaani lahaja hii huwa na watu wake maalum na sehemu maalumu ambao wazungumzaji wakuu wa lahaja hiyo.Kwa mfano lahaja ya Kimakunduchi huzungumzwa na watu wanaoishi Kusini mwa kisiwa cha Unguja (Makunduchi).

*Haina msamiati wa kimataifa (mawanda mapana):*Kutokana na sababu hii hatuwezi tukatumia katika shughuli za kitaifa kama vile bunge kwani hapatakuwa na mafahamiano kwa kuwa lahaja husemwa na kikundi cha watu.

*Huwa inatofautiana na lugha sanifu au lugha ya taifa:*Tofauti hii hujitokeza katika kipengele cha mofolojia (miundo),fonolojia (matamshi),sintaksia(sentensi)

na semantikia(maana).Kwa mfano katika lahaja ya Kimakunduchi hutamkwa *kiya* lakini katika lugha sanifu hutamkwa *kila*.Chum(2004).

Aidha tahajia ya lahaja ya Kimakunduchi yaani uwakilishi wake wa herufi zinazounda neno katika maandishi inatofautiana kutoka eneo moja na jengine.Kwa mfano wazungumzaji wa Kimakunduchi wanatofautiana katika kiimbo, sauti, mkazo na msamiati.Kama vile Kimakunduchi *afiki*,Kimtende *rafiki*, Kijambiani hutamka *afiki*.BAKIZA (2012).

Lahaja ya Kimakunduchi hufanana sana na msamiati wa lugha nyengine za kibantu. Hali hii ya kufanana imetokana na maingiliano ya muda mrefu kati ya wasemaji wa lahaja ya Kimakunduchi na wale wahamiaji waliokuja baadaye.Kwa mfano;

Jedwali Na 2.1: Kufanana kwa Misamiati ya Lahaja za Wahamiaji na Lahaja ya Kimakunduchi

Msamati wa Kimakunduchi	Fasili	Lugha
Ima	Simama	Kingozi
Uza	Uliza	Kingozi
Kale	Zamani	Kizigua
Sumka	Kimbia	Kihehe
Uka	Ondoka	Kimakonde

Chanzo: BAKIZA, 2012

Kutokana na jadwali la hapo juu linaeleza kufanana katika matumizi sawa ya maneno katika mawasiliano baina ya makundi hayo. Kwa mfano neno *ima* ina

maana *simama* katika Kingozi, neno *uza* Kimakunduchi ina maana sawa katika Kingozi *uliza*, neno *Kale* katika Kimakunduchi ina maana sawa ya *zamani* katika Kizigua, neno *sumka* Kimakunduchi inatumika sawa katika Kihehe kwa tendo la *kukimbia*, na neno *uka* Kimakunduchi ina maana ya ondoka katika Kimakonde. Maendeleo ya kielimu, sayansi na teknolojia na maingiliano ya watu katika jamii hiyo. Lahaja ya Makunduchi imepoteza baadhi ya maneno yake ya asili. Maneno kama vile “swi”, yaani *samaki* “kipangaa” yaani *kifuu*, tundu” , yaani vyakula mbali mbali vya matunda, hivi sasa hayatumiki.

Hivyo basi, ipo haja ya kufanya utafiti kutokana na mwachano na mwingiliano baina ya lugha na mfumo wa maisha ya jamii huenda vimechangia kuwepo kwa matumizi mbalimbali ya Mfanano na utofautiano wa utamkaji msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu na kuleta vikwazo katika mawasiliano baina ya makundi hayo mawili.

2.3 Kiswahili Sanifu na Usanifishaji Wake

Historia ya Kiswahili na usanifishaji wake. Katika kuilezea historia hiyo ameeleza kuwa kulikuwa na lahaja nyingi, lakini lahaja za Kimvita na Kiunguja ndizo zilizokuwa katika ushindani mkubwa katika mchakato wa kuteua lahaja moja ambayo itakuwa msingi wa Kiswahili sanifu. Hata hivyo pamoja na ushindani uliokuwepo hatimae lahaja ya Kiunguja ikateuliwa kuwa msingi wa Kiswahili sanifu. Mtafiti amependekeza kuwa ni muhimu katika utafiti wake kufahamu historia ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake ambayo imetoa mwangaza katika utafiti wake. Katika utafiti wake hakuonesha athari za Kiswahili sanifu katika

lahaja ya Kimakunduchi. Aidha hakuonesha jinsi athari hizo zinavyokwamisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi. Kazi ya Mbaabu Imemsaidia mtafiti kuwelewa usanifishaji katika Kiswahili. Mbaabu (1991). Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Tanzania. Kiswahili ni lugha yenye wazungumzaji wengi walioenea karibu Tanzania nzima, huzungumzwa kama lugha ya kwanza au lugha ya pili kwa wakaazi wote wa Tanzania (Mradi wa lugha za Tanzania, 2009).

Kiswahili kimeanza kuandikwa kwa hati za Kiarabu, watunzi wa mashairi waliandika mashairi kwa hati hizo. Wamishenari waliandika lugha ya Kiswahili kwa hati za Kilatini. Katika karne ya (19) Wajerumani na Waingereza walichunguza lugha hiyo Kyovi (2009).

Ludwing Krapf alichapisha kitabu chake mwaka (1854), *The Outline of Grammar of the Swahili Language*. Alitumia lahaja ya Kimvita, nae Steere akachapisha *Handbook of the Swahili as spoken in Zanzibar* mnamo mwaka (1870) akitumia lahaja ya Kiunguja. Hapo ikawa muhimu ni lahaja ipi itakayochaguliwa kuwa lahaja ya usanifishaji. Biblia iliyotumiwa na wahubiri, ilikuwa imetafsiriwa kwa lahaja ya Kiunguja na kulikuwa na kamusi katika lahaja hiyo. Wataalamu wa Kiswahili walitoa maoni yao. Mkutano wa kwanza wa mwaka (1925) ulifanyika Dar-es-Salaam ili kushughulikia suala la lahaja sanifu. Kati ya wawakilishi waliokuwemo ni Wamishenari-Church Mission to society na University Mission to Central Africa, wajumbe wa Serikali na Waandishi.

Vikwazo vilivyokuwepo mwishoni mwa karne ya (19) katika kuchagua lahaja moja ya kusanifiwa. Lahaja ya Kiunguja mjini ilisanifiwa na kupelekea kuibuka kwa Kiswahili sanifu na kilipewa hadhi ya kutumika katika sehemu za kazi, kwenye vyombo vya kutunga sheria, na maandishi yake ya utawala kwenye vitabu vya kitaaluma Mbaabu (1991).

Kamati na mabaraza yaliundwa kwa lengo la kukitetea Kiswahili sanifu (Maganga, 1997). Na hatimaye lahaja ya Kiunguja mjini ikasanifishwa katika kikao kilichofanyika mjini Mombasa mnamo mwaka (1928) na kufuatiwa na uundwaji wa kamati ya Kiswahili sanifu ya Afrika Mashariki KKAM mwezi Januari, mwaka (1930).

Islam (2009) ameeleza mnamo mwaka (1930), kamati maalumu, Inter-Territorial Language Committee iliundwa kwa madhumuni ya kushughulikia usanifishaji. Mwaka (1953), jina la baraza liligeuzwa na kuwa East Africa Swahili Committee. Mwaka (1964) kamati hii iligeuzwa na kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) chini ya chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Lengo kuu ni kukuza Kiswahili na kueneza matumizi yake katika viwango vyote nchini Tanzania, Afrika Mashariki na katika sehemu nyingine za Ulimwengu.

Miongoni mwa malengo ya kusanifisha Kiswahili ni kukuza na kupanua msamiati wa lugha. Kuelekeza utamkaji wa maneno yake, ilielekea kuwa baadhi ya lahaja za Kiswahili zilitofautiana sana katika utamkaji. Halikadhalika kuweka sheria zilizokubalika za matumizi ya lugha (sarufi). Vile vile kufuta tofauti

zilizokuwepo za kijamii, kijiografia, kiuchumi na kisiasa. Pia kuifafanua othografia ya lugha (hati) na etimolojia (asili) ya maneno yake.

Lugha ya Kiswahili hutumika nchini kote, katika utawala serikalini, mahakamani, makanisani, misikitini, redioni, na katika magazeti. Shughuli hizi hupatikana katika jamii ya Wamakunduchi waishio vijijini ambao hutumia Kiswahili katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Shughuli za utawala, ilifanya kazi ya kukiendeleza Kiswahili hadi vijijini vikiwemo vya Makunduchi kupitia mfumo wa utawala wa kutumia lugha hiyo Kyovi(2009).

Waingereza, waliwatumiwa wajumbe na Maakida katika kuwasiliana na wenyeji vijijini kwa ajili ya kuwatumia katika kazi zao, hali hii ilipelekea hata vijiji vya Makunduchi ilisaidia kuenea Kiswahili kwa shughuli kama hizi za utawala, hadi hii leo athari ya Kiswahili ipo kwani viongozi wa kata, shehia hutumia Kiswahili katika kazi zao na kutumia lahaja zao wakiwa katika jamii zao.

Mbali na shughuli za Kiutawala kuchangia kuenea kwa lahaja sanifu, shughuli za kisiasa zilichangia kwa kiasi kikubwa hadi vijijini /Kampeni za kudai uhuru kupitia chama cha ASP ziliendeshwa kwa lugha ya Kiswahili, hali hiyo ilisaidia sana kueneza Kiswahili hadi Makunduchi ambapo watu walijifunza na kuzungumza Kiswahili.

Kuwepo kwa vyombo vya habari kama vile redio na magazeti, vilisaidia kukieneza Kiswahili nchini Tanzania Whitely (1969). Watanzania wengi waliopo

vijijini wanamiliki redio ambazo husikiliza vipindi mbalimbali vinavyotangazwa kwa lugha ya Kiswahili. Wamakunduchi nao husikiliza vipindi hivyo. Hali hii ilisaidia kwa kiwango kikubwa kuathiri lahaja ya Kimakunduchi na wanavijiji vya Makunduchi kukielewa Kiswahili Sanifu. Hadi hii leo katika kijiji cha Makunduchi kipo kituo cha habari kilichopo kijiji cha Mtungujani-Makunduchi, kinarusha matangazo kwa kutumia Kiswahili sanifu. Pamoja na hayo shughuli za kielimu ilisaidia kutangaza Kiswahili sanifu.

Kwani hufundishwa mashuleni, vyo vikuu, na kuwa lugha ya mawasiliano katika maeneo hayo, kilitumika kusomeshwa katika ngazi ya msingi hadi sekondari. Makunduchi kuna shule nyingi kama vile skuli ya Makunduchi, skuli ya Kiongoni, Skuli ya Kusini na nyenginezo. Shule hizo huanzia msingi hadi sekondari ambazo hutumia Kiswahili sanifu wakiwa katika mazingira ya shuleni na husahau kabisa kuzungumza lahaja zao wakiwa darasani. Hali hii imechangia kuathiri lahaja ya Kimakunduchi zidi ya Kiswahili sanifu Palome (1980).

Athari za lahaja za Kiswahili katika Kiswahili sanifu zinaonekana bayana kwa namna mbali mbali lakini hakuna wataalamu wanaozizingatia kwa makini. Kutokana na maelezo haya yametupatia changamoto ya kufanya utafiti ili kuona lahaja ya Kimakunduchi ina athari gani katika Kiswahili sanifu.

2.4 Tofauti ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu

Kimakunduchi ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, kuna tofauti kubwa ya kimsamiati kati ya lahaja hiyo na Kiswahili sanifu. Tofauti inayojitokeza zaidi katika usanifishwaji. Kimakunduchi hakitumiki katika shughuli za kiserikali, na

kwa upande wa Kiswahili sanifu kimesanifishwa na kutumika katika shughuli za kiserikali. Tofauti nyengine katika maumbo ya maneno, ni utofauti wa msamiati katika maana na matumizi ndani ya jamii lengwa. Kwa hivyo mtu asiye kuwa Mmakunduchi ni vigumu kuelewa lahaja hii. Hii inatokana na utofauti uliopo kati ya msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja sanifu ya Kiswahili Juma, M (2011) Kwa mfano:

Jedwali Na 2.2: Tofauti Baina ya Lahaja Ya Kimakunduchi Na Kiswahili Sanifu

Kimakunduchi	Kiswahili Sanifu
Javi	Jamvi
Mahaa	Mahala
Toji	Tone
Kunguu	Kunguru
Muango	Mlango

Chanzo: Data za uwandani, 2016

Kutokana na jadwali la hapo juu linaonesha tofauti ya utamkaji baina ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu katika msamiati uliorodheshwa katika jadwali namba 2.2.

2.4.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi za Utafiti wa Kisayansi

Lahaja za Kipemba, Kiunguja mjini pamoja na Kiswahili sanifu. Utafiti wake ulijihusisha zaidi na kuelezea matamshi ya lahaja ya Kipemba, pamoja na kuzungumzia jinsi ukanushi unavyojitokeza ndani ya lugha hizo. Katika uchambuzi wake ametoa mambo mawili makubwa. Kwa kuanzia na msamiati kadhaa ya lahaja ya Kipemba na jinsi Kiswahili sanifu, na pia ameonesha

mabadiliko ya sauti mbali mbali na jinsi zinavyotofautiana kutoka maeneo ya mjini hadi vijjini..Aidha ameonsha umilikishaji wa lahaja ya Kipemba ambao kwa kiasi kikubwa kutokea ndani ya nomino husika kama:*nyumbayo* badala ya *nyumba yako*,*nduguyo* badala ya *ndugu yako*,*mtotongwa* badala ya *mtoto* wa watu.Pia alipendekeza kufanyike tafiti nyengine zinazohusu mabadiliko katika vitenzi.Kazi hii imemsaidia mtafiti katika kumuongoza kwenye utafiti wake hasa katika kuorodhesha msamiati wa Kiswahili sanifu. Mtafiti hakuonesha athari za lahaja ya Kimakunduchi katika lahaja ya Kiswahili sanifu.Mohammed (1984).

Historia ya Kiswahili na usanifishaji wake. Katika kuilezea historia hiyo ameeleza kuwa kulikuwa na lahaja nyingi, lakini lahaja za Kimvita na Kiunguja ndizo zilizokuwa katika ushindani mkubwa katika mchakato wa kuteua lahaja moja ambayo itakuwa msingi wa Kiswahili sanifu.Hata hivyo pamoja na ushindani uliokuwepo hatimae lahaja ya Kiunguja ikateuliwa kuwa msingi wa Kiswahili sanifu.Mtafiti amependekeza kuwa ni muhimu katika utafiti wake kufahamu historia ya lugha ya Kiswahili na lahaja zake ambayo imetoa mwangaza katika utafiti wake.Katika utafiti wake hakuonesha athari za Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi.Aidha hakuonesha jinsi athari hizo zinavyokwamisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi.Kazi ya Mbaabu Imemsaidia mtafiti kuwelewa usanifishaji katika Kiswahili Mbaabu (1991).

Lahaja tatu za Unguja,Lahaja hizo ni Kipemba,Kimakunduchi na Kitumbatu. Na kujumuisha Kiswahili sanifu kwa lengo kuu la kuchunguza mofofonolojia

ya lahaja ya Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu na kuzihusisha na Kiswahili sanifu. Katika utafiti wake aligundua kuwa asili ya Lahaja aliyoifanyia utafiti wake na alieleza jinsi zilivyotofautiana. Kutokana na utafiti wake alipendekeza kuwa lahaja hizo zifanyiwe tafiti za vipengele vyengine kama vile semantikia, sintaksia na morfologia. Kazi ya Maganga imemsaidia mtafiti katika kupata baadhi ya misamiati inayowiyana na inayotofautiana katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Maganga (1991).

Bakhresa (1992:44-265) ametafiti maana mbalimbali za kilahaja kwa kutumia Kiswahili sanifu. Katika uchunguzi wake amefanikiwa kutowa maneno baada ya uchunguzi wake katika lahaja mbalimbali. Mwandishi huyu ameangalia mifano ya lahaja ya Kitumbatu na Kimakunduchi kama ifuatavyo:

Kitumbatu neno *mumucha* hutamkwa *fyonza* katika Kiswahili sanifu. Pia neno *mfupa* katika Kiswahili sanifu hujulikana kwa neno *Muundi* katika lahaja ya Kitumbatu. Na kwa upande wa lahaja ya Kimakunduchi neno *Kiya* hutamkwa *Kila* katika Kiswahili sanifu.

Ulinganishaji wa sauti katika lahaja ya Kimakunduchi, Kijambiani na Kimtende na Kiswahili sanifu. Akimnukuu Chiraghadid na Mnyapala (1989) katika utafiti huo, wameeleza Kimakunduchi (Kikae au Kihadimu) ni lahaja yenye maneno mengi zaidi ya Kiswahili sanifu na machache ya lugha za kigeni, lahaja hii imefanana sana na Kijambiani kiasi mgeni anaweza kusema kuwa ni lahaja inayoshabihiana na Kipemba na lugha nyengine za

Kiswahili. Kutokana na utafiti huo alipendekeza kuwa kuchambua kwa kina misamiati inayohusu lugha ya Kiswahili sanifu au lugha nyengine. Utafiti huo umemsaidia mtafiti kuweza kubainisha misamiati inayotokana na asili ya lahaja ya Kimakunduchi Juma (2011).

BAKIZA (2012) wamefanya utafiti kuhusu msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi, wamekusanya msamiati na kuandika kamusi la lahaja ya Kimakunduchi, Kamusi la lahaja ya Kimakunduchi limekusanya msamiati kwa maeneo ya mbalimbali ya Makunduchi. Aidha walipendekeza taasisi nyengine za Kiswahili zifanye uchunguzi na kuandika kamusi za lahaja nyengine. Kazi ya BAKIZA ilimsaidia mtafiti kubainisha msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

Saleh (2013) alifanya utafiti kuhusu athari za kiisimu za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kinachotumika shuleni Makunduchi Zanzibar amezungumzia athari za Kimakunduchi na Kiswahili sanifu hususan katika maeneo ya kielimu tu. Kwa kubainisha sifa za kiisimu katika lahaja ya Kimakunduchi.

Kutokana na utafiti huu mtafiti alipendekeza kufanyike tafiti nyengine katika maeneo mengine kama shughuli za kilimo na kiutamaduni. Aidha utafiti huu ulimsaidia mtafiti kuelewa athari za kimatamshi za msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi.

2.4.2 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika miundo wa

kimawazo kwa mawazo ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo Massamba (2004).

Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani katika utafiti, nadharia ni muongozo ambao mtafiti atafuata ili kutekeleza kwa ufanisi utafiti wake (Kiswahili Sanifu (2013).

Katika utafiti huu tilitumia nadharia Makutano na Muachano ya Giles na Byrne (1982) iliyoelezwa na Massamba (2007: 72). Nadharia hii hufasiliwa mara nyingi kulingana na muktadha unaokusudiwa kutumika. Kwa namna ilivyokusudiwa nadharia hii hufanya kazi pale inapotokea jamii moja kutengana na nyengine na nyengine na kuendelea kutokea mabadiliko ya vipengele kadhaa vya kiisimu na hatimaye kutokea lugha tofauti, baadaye hufika wakati kila lugha ikazaa lahaja yake. Kwa upande mwingine lugha zilizokaribiana hufanana sana katika maumbo yake ya msamiati na kuwa lugha moja.

Massamba (keshatajwa) amefafanua nadharia ya mwachano na makutano ya lugha za Kibantu katika kueleza tofauti baina ya msamiati unaowiana kati ya lahaja ya Kimakunduchi na ile ya Kiswahili Sanifu, Chichifundi, Kipemba, na Chimwini katika kufananisha kwake ameeleza kuwa lahaja hizi inawezekana zilikuwa ni lugha tofauti za Kibantu lakini baada ya makutano na mahusiano ya muda mrefu lugha hizi zimetokea kuonekana kama ni lahaja za lugha moja. Kutokana na ufafanuzi wa nadharia hii imesaidia sana katika kuchunguza miongoni mwa athari za Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kwa wazungumzaji wa makundi

hayo mawili kukutana katika mazingira ya pamoja kwa mahusiano ya muda mrefu na kutokea lugha moja.

Katika kufafanua, Giles na Byrne (1982) wanaeleza kwamba msingi wa nadharia yake ya makutano kuhusu utambulisho wa jamii unategemea sana wazungumzaji lugha. Nadharia hii ya makutano inaeleza kwamba wazungumzaji wa jamii Y wanapofika hatua ya kuacha kuendelea kuzungumza lugha yao A katika mawasiliano yao ya kila siku na kuamua kuendelea lugha nyengine B ya jamii Z kwa lengo la kujinufaisha kijamii, kiuchumi, basi hali hiyo ikitokea tunasema, kumetokea makutano ya jamii mbili tofauti yaani, jamii Y na jamii Z zimekutana kwa kutumia lugha. Kimsingi, makutano hayo ya jamii husababisha athari hasi kwa jamii Y kwa sababu hatimae lugha yao A hupotea kwa kukosa wazungumzaji. Lugha A inapofikia hatua ya kupotea, basi utambulisho wa jamii Y na utambulisho wa wazungumzaji wa kudumisha lugha A pia hupotea kwa sababu ileile ya kukosa wazungumzaji wa kudumisha lugha A.

Kwa upande mwingine, nadharia ya mwachano iko tofauti na nadharia ya makutano iliyoelezwa hapo juu. Nadharia ya mwachano inaelezea kuhusu nguvu ya lugha kwa jamii K na jamii L kwa maana kwamba, kila jamii hutaka kuendelea kuzungumza na kudumisha lugha yake. Katika mazingira haya ambapo kila jamii huendelea kutumia na kudumisha lugha yake, huu ndio mfano wa kuwepo kwa mwachano wa jamii hizi mbili tofauti yaani, jamii K na jamii L. Kinyume na mfano wa makutano ya jamii mbili tofauti ambapo jamii moja huathirika kwa kupoteza lugha na utambulisho wake, mfano huu wa mwachano wa jamii hizi mbili, una athari chanya kwa maana

kwamba kila jamii yaani, jamii K na jamii L huendelea kutumia lugha yake na kudumisha utambulisho wa mzungumzaji na utambulisho wa jamii yake.

Msanjila (2011) anaeleza kwamba nadharia ya Giles na Byrne (1982) kusema kweli zinajaribu kuonesha siyo tu ukaribu wa uhusiano uliopo baina ya lugha na utambulisho, bali pia zinaonesha nguvu za lugha katika jamii jinsi zinavyotumiwa na wataalamu au wanajamii wenyewe kuweza kubainisha utambulisho wa mzungumzaji katika jamii yake.

Mzungumzaji yeyote asiyetumia lugha yake mara kwa mara katika mawasiliano ya kila siku, hupoteza umahiri wa kuzungumza lugha yake kwa kiwango cha mzawa wa lugha na kwa sababu hii husababisha utata wa kubaini utambulisho wake kwa kutumia kigezo cha lugha.

Utata hutokea kwa sababu vibainishi vya utambulisho wa mzungumzaji vinapopimwa kwa kuzingatia nadharia za Giles na Byrne za makutano na mwachano, huonesha kuwa nguvu ya lugha imepungua, hivyo wataalamu wa lugha hupata shida ya kuthibitisha utambulisho wake kwa vile hupelekea kutotumia misamiati inayowiana na inayotofautiana katika mazungumzo ya kila siku ni vikwazo vya kufikia mawasiliano fanisi. Msanjila (keshatajwa) amefafanua nadharia hii imesaidia sana katika kuchunguza miongoni mwa athari za Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kwa wazungumzaji hao inasemekana kuwa kuacha kwa lugha yake ya uzawa wake na kugundua kiini cha muachano.

Kwa kufafanua zaidi ,nadharia ya makutano katika misingi yake ya kinadharia inaaminika kuwa kuhusu utambulisho wa jamii unategemea sana wazungumzaji wa lugha.Yaani inapofikia hatua kwa wanajamii lugha kukubali kutumia lugha yao na kutumia lugha ya wanajamii wengine hapa tunasema kuwa na *makutano* lakini inapotokea jamii lugha zinazokaribiana kimaeneo, kila moja ikaendelea kutumia na kudumisha lugha ya mazingira kama hayo kwamba kuna *mwachano* wa jamii lugha.

Kutokana na utafiti huu nimetumia nadharia ya makutano na mwachano ya Gile na Byrne(1982) na ilionekana kutoa matokeo mazuri.Mkabala huu wa kinadharia unafaa kutumika kwa sababu unafafanua utambulisho wa nani anatumia aina fulani ya lugha,anatumia na nani katika muktadha gani, anatumia lugha zaidi ya moja.Nadharia hii imenisaidia katika utafiti wangu kujua vikwazo gani vinavyokwamisha mawasiliano kwa kundi gani katika jamii ya Wamakunduchi na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu kwa kutumia vipengele vilivyosaidia mtafiti katika kubainisha msamiati inayotumiwa na jinsi ilivyoathirika kwa kupitia makundi ya vijana,wazee,walimu na wanafunzi kwa ujumla.

2.4.2.1 Muhtasari

Sura hii ya pili ilichambua kwa kina mapitio ya kazi tangulizi zinazohusu lahaja kwa kutoa fasili ya lahaja ya Kimakunduchi,Kiswahili Sanifu na Usanifishaji wake, kama vile BAKIZA,Massamba,(wameshatajwa), Kiswahili Sanifu na usanifishaji wake kama vile Mbaabu, Kyovi , na kutoa tofauti ya Kiswahili Sanifu

na Kimakunduchi kama vile Juma, M (kashatajwa). Mwisho wa sura hii mtafiti alibainisha yale yanayohusu kiunzi cha nadharia ya mwachano na makutano ya Giles na Byrne (1982) kilichotumika katika utafiti huu.

.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii ilielezea mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data za utafiti huu. Sura hii iligawanywa katika sehemu saba. Sehemu ya kwanza, ilielezea usanifu wa utafiti, sehemu ya pili ilieleza muundo wa utafiti. Sehemu ya tatu ilielezea eneo la utafiti. Sehemu ya nne ilielezea sampuli na Usamplishaji. Sehemu ya tano ilielezea zana za utafiti, sehemu ya sita ilielezea mbinu za kukusanyia data (Usaili, hojaji na mbinu ya ushuhudiaji) na sehemu ya saba Uchambuzi wa data. Na sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura ya tatu.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Mkabala wa utafiti huu kwa sehemu kubwa ni wa maelezo. Cohen (2007) alieleza kuwa mkabala ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoenezwa na walengwa wa utafiti. Mtafiti huzipanga kutokana na maudhui au makundi yanayofanana. Mtafiti alikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, , kufanya majaribio, kutafsiri tarifa alizozipata kupitia mundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti huu ulitumia idadi ya watafitiwa kama ni kielelezo. Utafiti huu ulizingatia mkabala wa maelezo ambao kwa mujibu wa Mazhar (2013) unafafanua hisia, mawazo na mahusiano yanayoeleza namna na pahala, watu na matukio yalivyofanyika. Kwa kutumia mkabala huu wa maelezo ili kupata data zilizo katika maelezo katika dodoso na njia ya mahojiano lililoandaliwa na mtafiti kwa ajili ya kuchambua data kulingana na malengo ya utafiti.

3.3 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu una muundo wa sura tano. Sura ya kwanza ilieleza utangulizi kwa jumla na kujengwa na vipengele tofauti vikiwemo usuli wa tatizo kwa kufafanua fasili zilizohusu mada ya utafiti, sura ya pili ilieleza mapitio ya kazi tangulizi na kiunzi cha nadharia, sura ya tatu ilieleza mbinu za utafiti, sura ya nne uwasilishaji wa matokeo na majadiliano na sura ya tano hitimisho na mapendekezo. Sura hii ilielezea mkabala wa utafiti, muundo wa utafiti, mbinu za utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampilishaji, zana za utafiti, mbinu ya ukusanyaji wa data, na uchambuzi wa data. Nakumaliza na muhtasari wa sura hii.

3.4 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ni utafiti wa kitaaluma ya kiisimu ambapo ukusanyaji na uchambuzi wake wa data uliwasilishwa kinaelezo, kwa hiyo utafiti huu ulijikita katika mkabala usio wa kiutakwimu. Ubainishaji na ufafanuzi wa athari kwa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu na kutoa vipengele vinavyokwamisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa makundi hayo. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa njia sahihi ya kukusanyia data, kwa hiyo utafiti huu ulijikita kuchunguza athari za Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

3.4.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inahusisha uwasilishaji wa maswali kwa watafitiwa. Maswali yaliyojibiwa kwa njia ya mdomo na kujibu bila ya woga au hofu kulingana na ufahamu wao, na kurikodiwa kwa kinasa sauti, na kuandikwa kwenye daftari la kumbukumbu. Mbinu hii inaruhusu utoaji wa ufafanuzi inapogundulikana kama

taarifa fulani haijafahamika wakati wa kuuliza maswali. Pia husaidia kupatikana kwa taarifa za kina kwa kuweka ukaribu baina mtafiti na mtafitiwa (Kothari, 1990).

Kwa hiyo ,katika utafiti huu usaili umetumika ili kupata taarifa zinazohusiana na athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Pia, kupitia mbinu hii mtafiti amewauliza watafiti wake maswali ya aina moja na yapo mengine yanayotofautiana kwa kila kundi la watafitiwa ambao ni wazungumzaji wa Kimakunduchi, wakiwemo walimu 20, wanafunzi 20, wazee 20 na vijana 20 na jumla ya walengwa wote ni 80.

3.4.2 Mbinu ya Hojaji

Hojaji ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti ameaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani, Kothari (1990). Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemeana na taarifa inayohitajika mtu anayepewa hojaji hizo. Mbinu hii hutoa nafasi kwa mtafitiwa kujaza kwa muda wake na huweza kufanya shughuli nyengine binafsi bila ya kukwaza na hojaji na kupewa muda wa kuzirejesha hojaji hizo.

Hata hivyo baadhi ya watafitiwa hawarejeshi dodoso hizo au hawazijazi kabisa jambo ambalo ni hasara kwa mtafiti. Halikadhalika kwa udhaifu huu nimeutatuwa kwa katumia njia zaidi ya moja ya ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu mbinu hii nimetumia kwa kuwahoji walimu na wanafunzi walioteuliwa.

3.5 Mbinu ya Ushuhudiaji

Katika mbinu hii mtafiti ametumia kwa kushuhudia na kushiriki katika eneo la tukio, na vile vile asiweze kushiriki. Kwa mujibu wa (Kothari 2004:96-97) amefafanua kuwa ushuhudiaji ni njia ya kukusanyia data ya utafiti ambayo mtafiti hushuhudia tukio yeye mwenyewe bila ya kupewa taarifa na mtafitiwa.. Mtafiti ameweza kusikia mazungumzo ya lahaja ya Kimakunduchi na kurikodi kwa kutumia kinasa sauti alichokwenda nacho na kusikia na kuona matukio halisi. Kwa hivyo katika utafiti huu mtafiti amekwenda kijiji cha Nganani, Sokoni Makunduchi na kuona jinsi ya Kimakunduchi kinavyozungumzwa na kuweza kupata misamiati mingi ambayo hupelekea kukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji. Hivyo mtafiti amechunguza misamiati inayowiana, inayotofautiana na amegundua kuwa ndio chanzo kikuu cha kukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi kwa kupitia muktadha mbalimbali kama katika shughuli za kielimu, kilimo, sherehe za kimila, misiba na hata sherehe za harusi.

3.6 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Wilaya ya Kusini Unguja, eneo la Makunduchi. Wilaya imepakana na Jambiani kwa upande wa Kaskazini, Mtende kusini, Magharibi Kibuteni na kwa upande wa Mashariki bahari ya Hindi. Utafiti huu ulifanyika katika maeneo mbalimbali ya Makunduchi. Eneo la Kaskazini Kajengwa, Mtongani na maeneo ya Kusini yakiwemo Kusini, Tasani, Kaekuu na Sokoni. Uteuzi wa eneo hili umetokana na ukweli kwamba ndio kitovu cha lahaja ya Kimakunduchi, ni eneo linalozungumzwa lahaja hiyo. Aidha Wamakunduchi ni

weledi katika kutumia lahaja yao popote walipo. Hivyo, mtafiti alipata uthibitisho iwapo lahaja hiyo ilipata athari ambayo hukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kiswahili sanifu au Kiswahili sanifu huathiri na kupelekea vikwazo vya mawasiliano katika lahaja ya Kimakunduchi kwa kupitia shughuli mbalimbali za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

3.7 Sampuli na Usamplishaji

Kombo na Tromp (2006: 72) wanaeleza kuwa uteuzi wa sampuli ni utaratibu utumiwao na mtafiti katika kukusanya watu, mahali au vitu kwa ajili ya utafiti. Usamplishaji ni mchakato unaohusisha mbinu mbalimbali za uteuzi wa washiriki kutoka katika kundi kubwa ambalo hutumika katika kuwauliza kutokana na maswali ambayo yanatafutiwa jibu. Kothari (2004).

Mtafiti aliteua sampuli ambayo iliwakilisha majibu ya maswali yaliyolengwa katika utafiti huu. Sampuli iliteuliwa kwa kutumia kigezo cha umri, jinsia na kuchagua walimu na wanafunzi wa skuli za Makunduchi. Pia mtafiti alizingatia kuteua vijana na wazee ili kufikia malengo ya utafiti huu. Katika kupata taarifa za lahaja ya Kimakunduchi, mtafiti alihitaji kupata data ya kutosha na itayosadifu. Utafiti huu umetumia sampuli ya watu thamanini (80) ili mtafiti aweze kukusanya misamiati mingi. Sampuli hiyo imegawanywa katika makundi yafuatayo: wazee 20 wa umri kati ya miaka 50-80, wanafunzi 20 wa umri kati ya 15-18, walimu 20 kati ya 25 na zaidi, na vijana 20 kati ya miaka 25-38. Watafitiwa wote ni sawa na asilimia 80%, kutoka eneo la Kaskazini ikiwemo Kajengwa, Mtongani, Mtaandani na eneo la Kusini Makunduchi Tasani, Kaekuu, na

sokoni.Sampuli hii teule katika skuli ya Makunduchi, na skuli ya Kusini. Mtafiti ameteua sampuli hii ya wazee kwa sababu ndio wameweza kutoa taarifa za kiasili na kuifahamu vizuri misamiati ya zamani ambayo kwa sasa imeshapotea na ndio wazungumzaji wazuri wa lahaja hii ukilinganisha vijana ambao mtafiti ataangalia jinsi Kimakunduchi kinavyotumiwa na vijana vizazi vijavyo.Na sampuli ya walimu na wanafunzi kuona Kimakunduchi kama kinatumika katika shughuli za kielimu ama la.Halikadhalika kwa hayo,idadi ya sampuli yote itakuwa sawa sawa.Sampuli hiyo itakuwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na 3.1: Sampuli ya Watafitiwa Katika Maeneo Teule ya Makunduchi

Watafitiwa	Umri	Eneo la Kaskazini	Eneo la Kusini	Jumla
1.Wazee	Miaka 50-70	10	10	20
2.Vijana	Miaka 25-38	10	10	20
3.Walimu	Miaka 25-zaidi	10	10	20
4.Wanafunzi	Miaka 15-18	10	10	20
Jumla Kuu		40	40	80

Chanzo: Data za uwandani, 2016

3.8 Zana za Utafiti

Utafiti umetumia zana kama vile simu ya mkononi au kinasa sauti,daftari na kalamu,pamoja na hojaji,kinasa sauti kimemsaidia mtafiti kwa kunasa sauti za watafitiwa wake kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za uchambuzi wa data kwa wakati wa baadae.

Kalamu ,daftari,vifaa hivi vitanisaidia kwa kuandika baadhi ya taarifa muhimu zilizotolewa na watafitiwa,taarifa ambazo zimeandikwa kwa muhutasari,ambao umemuwezesha mtafiti kujua ni vipi aanze kuchambua data zake, na hatimaye

kuandika ripoti nzima. Pia karatasi za hojaji zitazoandaliwa na mtafiti zenye maswali na kuwapatia watafitiwa ambao wamezija kwa kutoa data ambazo zitafaa katika uandishi wa tasnifu hii.

3.9 Mbinu za Kukusanyia Data

Mtafiti ametumia mbinu tofauti za kukusanyia data .Katika kukusanyia data ni zoezi la awali katika utafiti.Kothari (1990) anaeleza kwamba katika hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya kupita katika hatua hii ya ukusanyaji data.Katika utafiti huu mtafiti amekusanyia data za msingi na za upili ambazo zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usaili,maswali ya hojaji ,ushuhudiaji,na majadiliano.

3.9.1 Data za Upili

Data za upili ni aina ya data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti.(Kothari,2008).Madhumuni hasa ya kukusanyia data hizi ni kujaliza data za msingi ili kusaidia kujibu maswali ya utafiti husika.Data hizi hukusanywa kutoka katika vitabu,makala,tasnifu,tovuti na wavuti.Ili kupata taarifa kupitia data hii ni lazima kupitia maktaba mbalimbali kutafuta maandiko yanayohusiana na mada husika. Maktaba nilizozitembelea ni pamoja na Maktaba ya tawi la Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania iliyopo Zanzibar,Maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania,Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar, na Maktaba kuu ya Taifa Zanzibar na Maktaba ya Baraza La Kiswahili Zanzibar.

3.9.2 Data za Msingi

Data za msingi ni data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake ya utafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa ajili ya utafiti kama huu uliofanywa hivi sasa. Data hizi zimekusanywa uwandani kutoka kwa watafitiwa mbalimbali ambao mtafiti amewateua kwa ajili ya kumpa data zitakazosaidia kujibu maswali yake ya utafiti Kothari (2008).

3.10 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia data zilizokusanywa kwa namna ambayo huezesha kukamilisha malengo ya utafiti husika. Uchambuzi wa data unahusisha na uhakiki na uainishaji wa data zilizokusanywa. Pia ni hatua muhimu ambayo husaidia kutafuta majibu ya tatizo la utafiti Babbie (1999).

Katika utafiti huu mbinu za uchambuzi wa data kama inavyoonekana katika sura ya nne ya utafiti. Mbinu hii inaelezwa kama mbinu isiyohusisha tarakimu bali ni maelekezo tu hutolewa katika kufafanua data ili kukamilisha malengo ya utafiti (Kothari, 2008).

Katika utafiti huu tarakimu zitatumika katika kubainisha misamiati, kutajia orodha ya majadwali, idadi ya watafitiwa kulingana majibu watakayotolewa baadhi huweza kukubali na wengine hukataa, hivyo ni wazi kutapatika mahesabu ya watafitiwa hao. Pia zitatumika tarakimu kwa kutegemea na maelezo ya watafitiwa. Katika

utafiti huu muna majadwali ambayo muna data ambazo zitachambuliwa kwa mbinu ya maelezo.

Pia uchambuzi wa uwasilishwaji huo utafanyika kwa kutumia nadharia ya mwachano na makutano ya Byrne na Giles (1982) kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu ili kupatikana taarifa zenye uhalisia kulingana na walengwa wa makundi ya lugha hizo.

3.11 Hitimisho

Sura hii imeelezea kiuhusu mkabala wa utafiti eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli zana za utafiti, mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya data na kuchambua data za utafiti zikiwemo, hojaji kwa kwenda katika vijiji vya Makunduchi ikiwemo Nganani, Sokoni (uwandani) na kutumia mbinu zaidi ya moja kama vile hojaji, dodoso na ushuhudiaji ambazo zilimsaidia mtafiti kuweka umakini katika uwekaji wa kumbukumbu zake na kumpatia data muafaka. Sura itakayofuata itajikita katika uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI MATOKEO NA MAJADILIANO

4.1 Utangulizi

Sura hii iliwasilisha matokeo ya utafiti huu juu ya uhusiano uliopo baina ya athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu na jinsi athari hiyo inavyosababisha kukosekana kwa mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Aidha sura hii inayachambua na kuyajadili matokeo hayo.

Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu tano zifuatazo: Sehemu ya kwanza, inaelezea taarifa za watafitiwa ili kufahamu sifa zao za kiisimujamii ambazo mtafiti amezitumia katika kufafanua na kutafsiri matokeo ya utafiti. Sehemu ya pili, inaelezea na kufafanua vipengele vya matamshi kwa kutumia kanuni za kifononolojia zinazotumika katika Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi.

Sehemu ya tatu, inaeleza na kufafanua athari za matamshi katika lahaja ya Kimakunduchi na kubainisha misamiati inayofanana na inayotofautiana. Sehemu ya nne inabainisha jinsi misamiati hiyo katika utamkaji wa asili na utamkaji wa sasa kwa lahaja ya Kimakunduchi. Sehemu ya tano, kufafanua mapendekezo juu ya kuondoa athari hizo, na sehemu ya sita ni muhtasari wa sura hii.

4.2 Taarifa za Kiisimujamii za Watafitiwa

Taarifa za kiisimujamii za watafitiwa katika utafiti huu ni kama Jedwali Namba 4.01 linavyoonesha:

Jedwali Na 4.1: Taarifa za Kiisimujamii za Watafitiwa

Watafitiwa	Eneo La Kusini	Eneo La Kaskazini	Asilimia
1.Wazee	8	8	20%
2.Vijana	10	10	25%
3.Walimu	10	10	25%
4.wanafunzi	12	12	30%
Jumla ya Watafitiwa Wote	NIL	80	100
Waliozaliwa Makunduchi	30	30	75%
Waliozaliwa Nje Ya Makunduchi	10	10	25%

Chanzo: Data za Uwandani, 2016

Utafiti huu wa lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathiriwa na Kiswahili Sanifu umetumia watafitiwa wenye sifa kama Jedwali Namba 4.01 linavyoonesha. Asilimia 20 ya watafitiwa ni wazee, asilimia 25 vijana, asilimia 25 walimu na asilimia 30 wanafunzi. Watafitiwa wote lugha mama ni Kimakunduchi. Data zimekusanywa katika eneo la Kusini na Kaskazini mwa Makunduchi. Taarifa zinaonesha kwamba asilimia 75 ya watafitiwa wote wamezaliwa Makunduchi na asilimia 25 ya watafitiwa hao wamezaliwa nje ya Makunduchi. Kwa ujumla, taarifa hizi za kiisimujamii ni taarifa za msingi kwa utafiti huu kwa sababu zimetumika kufafanua jamii ya Kimakunduchi na watumiaji wake.

4.2.1 Matumizi ya Kimakunduchi Kwa Jamii ya Wamakunduchi

Mtafiti aliweza kubaini matumizi ya Kimakunduchi kwa makundi ya kijamii ambayo mtafiti ameyachagua katika utafiti huu, wakiwemo wazee 20, vijana 20, walimu 20 na wanafunzi 20. Katika makundi hayo wapo waliokuwa wazawa na wasiokuwa wazawa. Mtafiti alibaini matumizi hayo kwa walimu na wanafunzi wakiwa

shuleni. Alitayarisha swali lake ambalo limewahusu wanafunzi (20) na walimu (20). Kati ya hao ni wa kidato cha pili na tatu, wanafunzi wote walijibu swali hilo isipokuwa wanafunzi wa tano tu, hawakulijibu. Swali liliulizwa hivi; 3) Je! Unazungumza Kimakunduchi ukiwa shuleni? Majibu yalikuwa hivi:

Jedwali Na 4.2: Uzungumzaji wa Kimakunduchi Shuleni

Walimu	Wanafunzi
25%	30%

Chanzo: Utafiti wa uwandani 2016

Matokeo yalikuwa kwa walimu ni asilimia 25%, na wanafunzi kwa asilimia 30%, imeonesha wanafunzi ndio waathirika wakubwa kwa kutumia lahaja ya Kimakunduchi katika maeneo rasmi. Kwa upande wa walimu wanahofia kuwa katika sheria za kazi zao hawaruhusiwi kutumia lakini wanafunzi hawana hofu yoyote ya kutumia lahaja hiyo, ndio maana wakawa na asilimia kubwa. Matokeo ya utafiti huu ilibainika kuwa matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi katika sekta rasmi hutumika kwa kiwango kidogo baada ya kuchunguza asilimia ndogo ya Walimu hutumia lahaja hiyo katika mazingira yasiyoepukika kwa sababu baadhi ya walimu ni wazawa wa eneo hilo wamepata athari katika lafudhi kwa mazungumzo ya kawaida ni vigumu kuepukika.

4.3 Kubainisha Msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili

Sanifu

Katika kipengele hiki mtafiti amewataka watafitiwa kubainisha msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Kabla ya kubainisha msamiati wa lahaja ya

Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Wikipedia(2016) inaelezwa kuwa Msamiati ni maneno yanayotumika katika lugha fulani. Hata hivyo, neno msamiati hutumika mara nyingi kumaanisha maneno yasiyojulikana na watu wengi, isitoshe “ *Msamiati hutumika kufafanua maana ya maneno yanayopatikana katika muktadha mbalimbali.*”

Msamiati hupatikana katika kazi mbali mbali, msamiati wa malipo, nyakati na saa, msamiati wa walemavu, msamiati wa mapambo na mengineyo kulingana na muktadha.

Kipengele hiki, kimejikita zaidi katika lengo la kwanza la utafiti huu ambalo lilimtaka mtafiti kubainisha msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu, Ili kuweza kufikia lengo hili, mtafiti alitayarisha swali na kuwapatia watafitiwa. Swali lilikuwa hivi; Naomba unipatie misamiati isiyopungua (20) inayotumika katika lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

Uchambuzi wa data zifuatazo umelijibu swali hilo. Utafiti umebaini kuwa wazee, vijana, walimu na wanafunzi wanatumia msamiati wa Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Data hizi zimekusanywa kwa njia ya usaili na hojaji.

Halikadhalika, katika kubainisha msamiati huo, mtafiti ametumia asilimia kufafanua watumiaji wa msamiati kutoka kwa watafitiwa wazee wamebainisha kwa asilimia 68%, vijana 45%, walimu na wanafunzi wote kwa asilimia 55%. Kwa hiyo asilimia ya wazee ni kubwa kulingana na vijana, walimu na wanafunzi, hii inamaanisha wafafanuzi wakuu na wanaotumia msamiati ni wazee. Hata hivyo mtafiti ameweza

kupata data katika ubainishaji wa msamiati hiyo, kwa kuigawa katika makundi kama vile msamiati inayohusu kazi mbalimbali, misamiati ya majina ya ukoo, msamiati wa walemavu, mapambo, mila/ utamaduni, msamiati wa malipo, pia msamiati wa saa na nyakati.

Jadweli Na 4.3.: Misamiati ya Lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu

Kimakunduchi		Kiswahili Sanifu
1	jua	jua
2	nyota	nyota
3	mbuzi	mbuzi
4	kibua	kibua
5	tandiko	godoro
6	maungo	mwili
7	mkoba	mfuko
8	kitanda	kitanda
9	mama	mama
10	bahari	bahari
11	mwisho	mwisho
12	sasa	sasa
13	ngalawa	ngalawa
14	nyoa	nyoa
15	sukuma	sukuma
16	tengeneza	tengeneza
17	tembea	tembea
18	tunasoma	tunasoma
19	dukani	dukani
20	sipitali	hospitali
21	ndoo	ndoo
22	kikohozi	kikohozi
23	buku	buku
24	kulala	kulala
25	njaa	njaa
26	saa	saa
27	cheka	cheka
28	kaa	kaa
29	Ruka	Ruka
30	Mkwezi	Mkwezi

Chanzo: Utafiti wa uwandani, 2016

4.4 Msamiati wa Kazi Mbali Mbali

Msamiati wa aina hii hupatikana kulingana na kazi mbali mbali ambazo Wamakunduchi na watumiaji wa Kiswahili Sanifu hushughulika nazo.

Jadweli Na 4.4: Msamiati wa Kazi Mbalimbali

Msamiati wa Kiswahili sanifu	Msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi
1-Karani	Mwandishi
2-Katibu	Mwandikaji
3-Mvuvi	Mchuuzi
4-Mhasibu	Mvelekaji
5-Bwanashamba	Mkulima
6-Daktari	Tabibu
7-Mhandisi	Fundi muashi
8-Mkutubi	Mkutubi
9-Tabibu	Mlyaji
10-Mfinyanzi	Mpondaji

Chanzo: Data za uwandani, 2016

Mifano iliyopo katika jadweli 4.5 linaonesha msamiati iliyotumika katika kazi mbalimbali kwenye Kiswahili Sanifu na Kimakunduchi.

4.5 Misamiati ya Nambari za Msingi

Haya ni majina ya tarakimu mbalimbali zinapoandikwa kwa herufi. Misamiati ya nambari hizi hupatikana katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu kama zinavyoonekana katika Jedwali Na. 4.5.

Mifano ya msamiati wa nambari za msingi katika jadweli 4.6 linaonesha nambari za msingi ambazo zinawiana kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

Jadweli Na 4.5: Msamiati wa Nambari za Msingi

Tarakimu	Kiswahili sanifu	Kimakunduchi
0	Sufuri	Sufuri
1	Moja	Moja
2	Mbili	Mbili
3	Tatu	Tatu
4	Nne	Nne
5	Tano	Tano
6	Sita	Sita
7	Saba	Saba
8	Nane	Nane
9	Tisa	Tisa
10	Kumi	Kumi

Chanzo: Data za uwandani, 2016

4.6 Msamiati wa walemavu

Haya ni majina wanayopewa watu wenye ulemavu wa sehemu mbalimbali za mwili, kiungo cha mwili ,kusemekana kwamba kumelemaa pale ambapo hakiwezi kufanya kazi zake vizuri kama inavyohitajika.Kwa mfano macho yasiyoweza kuona chochote,miguu isiyoweza kutembea na mengineyo.

Jadweli Na 4.6: Msamiati wa Walemavu

Lahaja Sanifu	Kimakunduchi
Bubu	Kusichoweya
Chongo	Kusikona
Kibogoyo	Kusimeno
Kigugumizi	Kigugumizi
Kiwete	Kiwete
Kipofu	Msiona
Kiziwi	Mziwi
Matege	Matege
Gumba	Magumba
Kilema	Kilema
Chongo	Kusiona

Chanzo: Data za uwandani, 2016

Katika jadweli 4.6 linaonesha msamiati wa walemavu ambao hupatikana katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

4.7 Msamiati ya Majina ya Ukoo

Msamiati ya majina ya heshima yanayotumiwa na watu mbalimbali katika familia kulingana na uhusiano wao. Pia huitwa msamiati wa unasaba.

Jadweli Na 4.7: Msamiati ya majina ya ukoo

Misamiati ya Kiswahili sanifu	Misamiati ya Kimakunduchi
Baba	Bwana
Mama	Bimkubwa
Mtoto	Mwanakele
Kaka	Kaka
Dada	Dada
Mtoto wa kwanza	Kifungua mimba
Kitinda mimba	Mwanaya mwisho
Mke	Mke
Mume	Mume
Mjomba	Mjomba
Babu	Babu
Bibi	Bibi
Mjukuu	Mjukuu
Mtoto wa mjukuu	Kilembwe
Wifi	Pande
Mkwe	Mkwe
Kitikuu	Kituguu
Kinyinginya	Kinyinginya
Mapacha	Mapacha

Chanzo; Data za uwandani, 2016

Mifano ya msamiati iliyotolewa katika jadweli 4.8 linaonesha msamiati ambao unapatikana katika majina ya ukoo/ unasaba ambayo hutumika kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

4.8 Msamiati ya Mapambo, Mila na Utamaduni

Msamiati ya aina hii hupatikana katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu na kutumika katika mapambo, mila na utamaduni wa jamii husika.

Jadweli Na 4.8: Msamiati ya Mapambo, Mila na Utamaduni

Kiswahili sanifu	Kimakunduchi
Bangili	Bangiri
Cheni	Kidani
Pete	Pete
Poda	Podari
Herini	Herine
Usinga	Usinga
Mafuta	Mafuta
Marashi	Marashi
Hina	Hina
Ukaya	Ukaja
Wanja	Wanja
Winda	Winda
Kipini	Kipini
Seruni	Seruni
Kungwi	Kungwi
Mshipi	Utali
Ushanga	Tunda
rangi ya mdomo	Rangi ya mdomo
Chetezo	Chootezi
Sanda	Sanda
Ubani	Ubani
Udi	Udi

Chanzo: Data za uwandani, 2016

Katika jadweli 4.9 linaonesha mifano ya msamiati wa mapambo, mila na utamaduni inatumika katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

4.9 Msamiati ya Nyakati

Msamiati ya nyakati ni aina ya msamiati ambayo hupatikana kwa kuzingatia nyakati kutokana na kubadilika kwa siku, saa, na nyakati.

Jadweli Na 4.9: Msamiati Ya Nyakati

Kiswahili Sanifu	Kimakunduchi
Leo	Leo
Jana	Jana
Juzi	Juzi
Kesho	Kesho
Keshokutwa	Keshokutwa
Mtondogoo	Mtondogoo

Chanzo; Data za uwandani, 2016

Mifano ya hapo juu katika jadweli 4.10 linaonesha misamiati ya nyakati ambayo hutumika kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

Jadweli Na 4.10: Misamiati Ya Masaa Ya Siku

Kiswahili Sanifu	Kimakunduchi
Asubuhi	Asubuhi
Mchana	Mchana
Usiku	Usiku
Jioni	Jioni
Adhuhuri	Adhuhuri
Alasiri	Laasiri
Mawio	Ulejua
Machweo	Uchwejua
Usiku wa manane	usiku wa maneno

Chanzo: Data za uwandani, 2016

Katika jadweli 4.11 ,mtafiti amebainisha msamiati wa masaa ya siku ambayo hutumika katika mawasiliano ya kila siku.

4.10 Msamiati ya Malipo

Katika utafiti huu zimekusanywa data kwa njia ya mahojiano, dodoso kupitia kwa walengwa ambao walikuwa ni walimu 20, wanafunzi 20 , wazee 20 na vijana 20 ambao wamepatikana katika maeneo ya Kaskazini na maeneo ya Kusini

Makunduchi ikiwemo skuli ya Makunduchi, skuli ya Kusini na vitongoji vyake. Mtafiti amekusanya data kwa lengo la kubainisha misamiati inayowiana, inayotofautiana, misamiati ambayo mingine hukwamiza mawasiliano kwa watumiaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu.

Jadweli Na 4.11: Msamiati ya Malipo ya Kifedha

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU
Wajibu	Ada
Nauli	Nauli
Marupurupu	Marupurupu
Fidia	Fidia
Faraga/chauchau	Rushwa
Kinua mgongo	Mafao

Chanzo: Uwandani, 2016

Mifano ya hapo juu katika jadweli 4.12 linaonesha msamiati ya malipo ambayo hutumika katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.

Katika kipengele hiki mtafiti amebainisha msamiati kama ilivyojidhihirisha katika jadweli zilizotangulia watafitiwa wameweza kubainisha msamiati hiyo kwa kuainisha katika makundi ya aina za maneno katika jadweli namba (03), msamiati ya kazi katika jadweli namba (04), msamiati ya nyakati na saa kama inavyodhihirika katika jadweli namba (09), msamiati ya mapambo, mila na utamaduni katika jadweli namba (08), msamiati ya watu wenye ulemavu kama ilivyodhihirika katika jadweli namba (06), na msamiati ya malipo ambayo hudhihirika katika jadweli namba (11).

Kwa ujumla wa matokeo ya data hizi ni dhahiri kuwa msamiati imebainishwa kwa kiwango kikubwa hasa kwa wazee ndio watumizi wazuri wa msamiati. Kwa kiwango kidogo sana msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi hufanana na Kiswahili sanifu, na kiwango kikubwa hutofautiana kulingana data zilizopatikana katika utafiti huu. Hivyo utofauti wa msamiati hiyo ndio chanzo kikuu cha kukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu hatimae huleta athari kama itakavyoelezwa hapo chini.

4.11 Athari Za Lahaja Ya Kimakunduchi

Katika utafiti huu lengo mahususi ni kuchunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika misamiati ya Kiswahili sanifu. Ili mtafiti aweze kufafanua lengo hili, mtafiti aliwauliza maswali watafitiwa maswali yafuatayo:

- i) Je, lahaja ya Kimakunduchi imekutwa na athari yoyote?
- ii) Kwa kiasi gani matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi yanaathiri matamshi ya lahaja sanifu?

Utafiti huu ulipima namna ya msamiati ilivyoathirika kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Maoni ya watafitiwa katika utafiti huu yalikuwa ya kujaza dodoso.

Jadweli Na 4.12: Athari za lahaja ya Kimakunduchi

Watafitiwa waliohojiwa	Msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi	Matamshi Yaliyoathirika	Matamshi ambayo Hayakuathirika
80	60	√	
	40		√

Chanzo: Data za Uwandani, 2016

Ukichunguza jadweli kielelezo Namba(5.2) Utaona kuwa jumla ya watafitiwa 80 sawa na asilimia (100%) iliyoapatikana katika eneo la Kusini na Kaskazini Makunduchi walioshiriki katika kujibu swali lililolenga kuchunguza athari za msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi katika shughuli za kijamii kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Pia utagundua kuwa jumla ya msamiati yalikuwa yakipima lengo hili ambapo jadweli hapo juu linaonesha kuwa maoni ya watafitiwa yanabainisha kuwa msamiati 60 yamepata athari kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kiswahili sanifu na maneno 40 ndiyo hayakuathirika. Hivyo matokeo ya utafiti huu yanadhihirika kuwa msamiati mingi imepata athari kutokana na asilimia kubwa ilivyoainishwa na watafitiwa.

Vielelezo vya majadweli yafuatayo yanabainisha msamiati inayotumika katika shughuli za kijamii ambayo hutumiwa na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi yalivyobainishwa na watafitiwa wa utafiti huu nakuonekana jinsi ilivyopata athari hasa katika matamshi.

Athari hizo zinaweza kuwa hasi au chanya. Hata hivyo athari zilizo bainika ni hasi. Hivyo zilichunguzwa athari katika makundi mawili kama ifuatavyo:

- i) Katika matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi
- ii) Katika matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi.

Athari katika matamshi: Ifuatayo ni orodha ya misamiati iliyobainisha athari katika matamshi ,ambayo imefuata vipengele /kanuni za kifonolojia kama vile udondoshaji, ubadilikaji wa kiumbo ,uingizaji kwa baadhi ya msamiati wake ukilinganisha na Kiswahili sanifu.

4.12 Udondoshaji wa Nazali katika Msamiati

Kimakunduchi hudondosha nazali katika msamiati wake, wakati nazali (n na m) zinapokutana na sauti [pj] na kikwamiza [ʃ] na nazali kama vile [ɲ] hubadilika msamiati wake.

Pia hudondosha nazali zinapofuatana na baadhi ya msamiati ulioanzia na vikwamiza ghuna kama vile [z], na [v].

Kwa mfano, neno mnyama- hutamkwa nyama, mpya –hutamkwa pya, mvua- hutamkwa vua, nchi- hutamkwa chi, nzi- hutamkwa zi.

Udondoshaji huu umepelekea kukwamiza mawasiliano na kuleta athari kwa wazungumzaji wa makundi haya mawili kutopata mafahamiano katika mazungumzo yao. Umejitokeza katika jadweli lifuatalo hapo chini:

Katika neno mnyama imedondoshwa nazali /m/, nakutamkwa **nyama**, pia neno **mpya** na kuwa **pya**. Katika neno mvua imedondoshwa nazali /m/ nakutamkwa **vua**, neno hili huzua utata kwa mtumiaji wa Kiswahili sanifu hufahamu ni kitendo cha kuvua nguo au vua samaki. Katika neno **nchi** imedondoshwa kikwamiza /Ch/

Jadweli Na 4.13: Udondoshaji wa Nazali Katika Misamiati

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
Nchi	Chi
Mnyama	Nyama
Mpya	Pya
Jamvi	Javi
Mvua	Vua

Chanzo; Data za Uwandani, 2016

4.13 Udondoshaji wa Kilainisho/ l/ na Kimadende / r/.

Kwa upande mwengine Kimakunduchi hudondosha kilainisho /l/ na kimadende /r/ na kuingiza irabu wakati sauti hiyo inapotanguliwa na irabu /a, u na i/ Kimakunduchi kinapoondosha sauti hizo ama hufanya irabu mbili zifuatane au hufanya irabu ndefu kama inavyojionesha katika maneno yafuatayo:

Jadweli Na 4.14: Udondoshaji wa Kilainisho l/ na Kimadende / r/

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
Harusi	Ha –usi
Vuruga	Vu –uga
Kunguru	Kungu-u

Chanzo: Data za Uwandani, 2016

Katika neno harusi imedondoshwa kimadende/ r / nakuwa hausu. Pia katika neno vuruga imedondoshwa /r/na kuwa vuuga.

Katika neno kunguru imedondoshwa kimadende /r / na kuwa kunguu.

Udondoshaji huu unapelekea athari zinazokwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa Kimakunduchi.

Kwa hiyo data alizopata mtafiti zinaonesha kuwa msamiati uliotajwa katika jadweli 4.15 imefuatwa na kanuni ya udondoshaji imeibadilisha umbo la ndani kutoka (ha –ru-si) na kuwa (ha-u-si), (vu-ru-ga) na kuwa (vu - u- ga), msamiati (ku-ngu-ru) na kuwa (ku –ngu- u).

Udondoshaji wa konsonanti /r// katika mazingira ya kufatiliwa na irabu /u/ hubadilika, na kudhoofika kwa konsonati za Kiswahili Sanifu ni:

/r/ → [u] / - / u /.

4.14 Uingizaji wa Sauti -y-, pamoja na Uingizaji wa Sauti kuwa -lya-

Data zinaonyesha kuwa uingizaji wa sauti -y- na lya- hujitokeza katika sehemu tofauti ya neno katika lahaja ya Kimakunduchi, kama jadweli lifuatalo linavyoonesha hapo chini:

Jadweli Na 4.15:: Uingizaji wa sauti-y-, na kuwa -lya-

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU
Nyiuza	Niulize
Tulye	Tule
Nyongeza	Niongeze
Yulya	Yule
Vilyavilya	Vilevile

Chanzo; Data za uwandani, 2016

Katika neno niulize na niongeze imeingizwa sauti / ny/ nakubadili neno katika umbile lake la awali na kuwa / nyiulize/ na / nyongeza. Halikadhalika uingizaji wa -ly- katika neno vilyavilya na yulya kwa (Kimakunduchi) kwa neno vilevile na Yule (Kiswahili Sanifu).

Data hizi zinaonesha athari ya mawasiliano katika makundi mawili baina ya Wamakunduchi na watumiaji wa Kiswahili sanifu. Makundi hayo yanapokutana katika mazungumzo huwa hawafahamiani kwa sababu ya uingizaji wa sauti kama /y/ na /ly/.

Kutokana na jadweli la 4.16 katika kanuni ya uingizaji wa nusu irabu /j/ na kupelekea mabadiliko ya kudhoofika kwa konsonati ikifuatiwa na irabu //e/

huingizwa /j/ katika neno (yu-le) na kuwa (yu-lya) na irabu /o,i/ katika neno (ni –o-nge-ze) na kuwa (nyi –o –nge- ze),Uingizaji huu hubadilisha umbo la neno na mtafiti amegundua kutokana na data alizozipata kutoka kwa walengwa na kupata kanuni :

/j/ →[ɟ] / - / a/.

Katika Kiswahili Sanifu, nusu irabu /j/ imebadilika umbo katika mazingira ya kutanguliwa na kimadende /l/ na kuingizwa /j/ na / a/..

4.15 Uingizaji wa Sauti/ nch /,k/,j / ,/w /.

Data zinaendelea kuonesha kuwa uingizaji sauti/ nch/,/ k/, /j/ ,/w/ hizo katika Kimakunduchi umeleta athari ya ukwamizaji wa mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu kama unavyojidhihirisha katika jaduveli hapo chini. umeweza kubadili kipasuo / g/ kuwa kizuiwa kwamizwa /j/ , hivyo Kimakunduchi hutumia kipasuo /g/ katika neno gino badala ya kizuiwa kwamiza /j/ inayotumika katika neno jino.Vile vile ubadilikaji wa kikwamiza /tʃ/ kuwa kipasuo /t/,Kimakunduchi hubadilisha kipasuo /t/ katika neno taka-**ch**aka, ntakupiga-**nch**akupiga, katika neno nauza imeingizwa kipasuo /k/ nakuwa nakuza .

Katika neno jino(Kiswahili Sanifu) limebadilika umbo kwa kuingizwa kipasuo / g/ na kuwa gino.Pia uingizaji wa kiyeyusho /w/ nako kumefanya ubadilikaji wa umbo la neno, kwa mfano kuimba(Kiswahili sanifu) imekuwa kwimba(katika Kimakunduchi).

Jadweli Na 4.16: Uingizaji wa Sauti /nch/, /k/ na /w/

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
Nitakupiga	Nchakupiga /ch/
Nauza	Nakuza /k/
Nataka	Nnachaka
Kuimba	Kwimba /w/
Taka	Chaka /ch/

Chanzo: Data za Uwandani,2016

Katika jadweli 4.17 linaonesha uingizaji wa sauti /tʃ /, /k/, /j/ na /w/. mabadiliko ya sauti kipasuo /t/ imeingia vizuiwa kwamizi kama vile msamiati wa neno (ni-ta-ku-pi-ga) na kuwa (n-cha-ku-pi-ga). pia neno (ta -ka) imekuwa (cha-ka), mabadiliko yenyewe ni :

/t/ → [tʃ] -/ n/

Vile vile uingizaji wa nusu irabu kumebadili umbo la msamiati ,umbo la ndani (kuimba) , na umbo la nje (kwimba). Irabu /i/ na / u/ hukumbwa na badiliko na kuwa nusu irabu kama msamiati ulionesha katika jadweli 4.17:

/ u / → [w] -/ i/.

4.16 Uingizaji wa Sauti /v/ na / vy /katika Lahaja ya Kimakunduchi

Data zifuatazo zinaonyesha kuwa uingizaji wa sauti / v/ na /vy/ katika Kimakunduchi hupelekea athari ya kutokufahamiana baina ya makundi hayo kaitika mawasiliano .Kwa mfano, neno pakata (Kiswahili) limekuwa vyakata(Kimakunduchi) neno pokea limekuwa vokea (Kimakunduchi), Neno pita (Kiswahili sanifu) limekuwa vita ,msamiati huu umezidi kuleta athari kwani wazungumzaji wa Kiswahili sanifu

hufahamu kama vita au mapigano baina ya nchi na nchi ,badala ya kuelewa kitendo cha kupita ndani.

Jadweli Na 4.17: Uingizaji wa sauti /v/ na /vy/.

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
Pakata -p-	Vyakata –vy-
Pokea -p -	Vokea –v-
Pita -p-	Vita -v -
Mwizi -z-	Mwivi –v-
Anapita -p-	Kanavita –v-

Chanzo: Data za Uwandani,2016

Katika jadweli 4.18 linaonesha uingizaji wa sauti /v/ na / vy/, sauti /z/ na /v /, sauti /p/ na /v/.

Kutokana na data alizozipata mtafiti zinaonesha kuwa Kimakunduchi kimepata athari katika matamshi ambayo yameweza kubadili ombo la msamiati ,Kwa mfano kutokana na neno (pa-ka-ta) tumepata neno (vya- ka-ta) ,msamiati (po-ke-a) tumepata neno (vo-ke-a), neno (pi-ta) tumepata neno (vi-ta) ambalo linaonesha utofauti wa kiumbo na kimaana kati ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu.Tuangalie badiliko lenyewe:

- /p/ →[v] /- / a/

Hapa tunaona sauti /p/ imepoteza sifa ya kuwa kipasuo sio ghuna na kuwa kipasuo ghuna / v /

- /z/→ [v] / - / i/

Hapa kutokana na sauti /z/ kipasuo cha ufizi kimepata badiliko la kutanguliwa katika mazingira ya irabu /i/ katika msamiati uliopo katika jadwali 4.18, konsonanti imedhoofika na kuwa konsonanti ya mkwaruzo /z/ katika mazingira ya kutangulia vokali/i/.

4.17 Athari za Kiumbo

Data zimebainisha kuwa zipo sauti za misamiati zinatofautiana baina ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ambazo hubeba athari za kiumbo kama zinavyoonekana katika jadwali lifuatalo hapo chini. Data hizo ambazo zimeonekana kupata mabadiliko ya kiumbo kutokana na neno lake la asili.

Jadwali Na 4.18: Athari za Kiumbo

KISWAHILI SANIFU		KIMAKUNDUCHI
i.	Yanatoka	Yanalawa
ii.	Nipe	Nka
iii.	Zungumza	Chowea
iv.	Kapotea	Kaga
v.	Kukosha	Kosa
vi.	Nimeisha	Nyisi
vii.	Sikubali	Sidumbu
viii.	Sijui	Siviji
ix.	Kuoga	Koga
x.	Mtoto	Mwanakele
xi.	Twenzetu	Twenende
xii.	Ondosha	Wisha
xiii.	Jasi	Fusi
xiv.	Mkeka	Bacha

Chanzo: Eneo la Kaskazini Makunduchi, 2016

Kutokana na maelezo yote ambayo mtafiti ameyapatia ufafanuzi kwa kuangalia zaidi misamiati baina ya Kiswahili sanifu na Kimakunduchi ,imegundulika kuwa Kimakunduchi kimeathiri sana kwa wazungumzaji ambao si wazawa walahaja hiyo na kupelekea kukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji hao.

Athari katika matumizi ya lahaja ya Kimakunduchi: Data zifuatazo zinaonesha kuwa watafitiwa waliojibu swali la kuonesha athari za lahaja ya Kimakunduchi kama jadweli (12) linavyoonesha hapo chini:

Jadweli Na 4.19: Athari katika Matumizi ya Lahaja ya Kimakunduchi

WAZEE 65%	Vijana 45%	Walimu75%	Wanafunzi 60%
1-Maneno mengi yenye asili ya lahaja hio yameachwa.	-Utumiaji wa Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari na kuachwa lahaja ya Kimakunduchi.	-Wageni kuingiza lugha zao.	-Matamshi
2-Maneno mapya	-Lafudhi	-Kutokutumika katika shughuli	
Yasiyokuwa na asili yameingia		Rasmi.	
3-Kusahaulika kwa vitu vya asili ,kwa mfanoKiwe-jiwe la			
Kusagia nafaka.			

Chanzo; Data za Uwandani, 2016

Utafiti umebaini kuwa wazee wametoa athari kwa asilimia 65%,vijana wametoa asilimia 45%,walimu wamepata asilimia 60%.Data zimepatikana uwandani kwa njia ya mahojiano na dodoso kama zinavyojidhihirisha hapo juu.

4.18 Matamshi ya Kimakunduchi Yanavyoathiri Kiswahili Sanifu

Matamshi /Sauti ni tawi la sayansi ya isimu,inayoshughulikia uchunguzi wa mfumo wa sauti katika lugha fulani,kwa mfano katika ugawaji wa irabu na konsonanti,ala za sauti katika utamkaji wa fonimu katika lugha za binaadamu.Katika matamshi hujikita katika matamshi,masikizi na hata kasoro za matamshi ambazo huwa za kimaumbile ambazo huathiri utamkaji wa sauti za maneno.(Massamba,2004).Halikadhalika katika utafiti huu utaonesha athari ambazo hujitokeza katika mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kimakunduchi na Kiswahili sanifu vikiwemo vigezo vya lafudhi,kiimbo,kidato, pamoja na sauti/vitamkwa zaidi kwa kuangalia misamiati hukwamiza mawasiliano na kupelekea kutokufahamiana baina ya wazungumzaji hao.

Kwa kuanzia na Lafudhi,ni ule upekee wa mtu katika matamshi unaathiriwa na lugha mama,mazingira yake ya kijiografia au kiwango cha ujuzi wake wa lugha.Kiswahili kina lahaja tofauti kama vile Kimakunduchi,Kilamu na nyenginezo.Tofauti kubwa ni misamiati,muundo wa sentensi, au matamshi.

Pia kwa upande wa Kiimbo huweza kuleta athari katika misamiati ya makundi haya mawili,ikiwemo Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ambapo hali ya usemaji wa mtu kwa kawaida hutambulisha toni na mkazo.Katika kiimbo kuna toni za hali ya kuuliza ,kusimulia, kushauri na kuamrisha.

Kwa mfano Unasemaje? Unasemaje!. Kwa upande wa Kitamkwa ni sauti dhahiri inayosikika wakati wa utamkaji wa maneno na ambayo inatambulika

kialfabeti, kama vile p, b, d, k, g, f na nyenginezo. Kwa mujibu wa Maganga keshatajwa, anabainisha sauti za Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Miongoni mwa sauti alizozibainisha hazijitokezi katika msamiati wa Kimakunduchi ambao umechunguzwa. Sauti hizo ni [θ], [r], [ʏ], na [ð].

Kwa mujibu wa utafiti huu Lahaja ya Kimakunduchi kama zilivyo lahaja nyingine za Kiswahili Sanifu kina sauti nyingi zenye kulingana na Kiswahili sanifu lakini hakina sauti kadhaa ambazo zina asili ya lugha ya Kiarabu ambazo nimezirodhesha hapo awali. Data zetu za utafiti huu Kimakunduchi kina sauti zifuatazo:

Konsonanti: [p], [b], [t], [d], [g], [k], [ʃ], [f], [v], [s], [z], [h], [m], [n], [ɲ], [ɳ].

Viyeyusho: [w], [j]

Irabu: [ɛ], [i], [ɔ], [a], [u], [u:], [a:], [i:], [ɛ:].

Hebu tuangalie Jedwali Na 4.21 lenye kuonesha sauti/matamshi ya Kimakunduchi ya konsonanti na nusu irabu.

Kutokana na sauti ambazo zimejitokeza katika jadwali Na 4.21 imebainika kuwa kuna konsonanti ambazo hujenga neno kwa kuingizwa kwa nusu irabu ambazo ni /w/ na /y/ huonesha athari ambayo hujitokeza katika lahaja ya Kimakunduchi kwa kuwaangalia wazungumzaji wa lahaja hiyo hutofautika na Kiswahili sanifu, kwa kutumia kiimbo, kidatu na kwa baadhi ya maneno hutumia mkazo na orodha yote ya

konsonanti zilizokuwemo katika jadweli hilo ukitoa nusu irabu /w/, na / y/,Kwa mfano neno kukataa-husema **taa**:huvuta Kwa ishara ya kuwa hataki kabisa

Jedwali Na 4.20: Konsonanti na Nusu Irabu za Kimakunduchi

Namna ya utamkaji	Mahali pa kutamkia						
		Midomo	Mdomo Meno	Ufizi	Kaakaa Gumu	Kaakaa Laini	Glota
Vipasuo	Sighuna	P	T			k	
	Sighuna mpumuo	p ^h	t ^h			k ^h	
Kizuiwa kwamizwa	Sighuna				tʃ ^h		
	Sighuna mpumuo				tʃ, f		
Kikwamizwa	Sighuna		ʃ	s	ʃ		h
Nazali		m		n	ŋ	ɲ	
Vilainisho	-Siguna						
	-Ghuna				j	w	

Chanzo: Massamba na wenzake (2004: 44)

Kwa hivyo kutokana na utafiti huu mtafiti amebaini kuwa matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi yamepata athari katika mawasiliano na kuonekana yameathiri matamshi ambayo hutumika ndani ya jamii na huwa tofauti na matamshi ya Kiswahili sanifu, utamkaji wake, ubadilikaji wa miundo ya misamiati na sentesi, maana na matumizi ya maneno imegundulika katika utafiti huu ukilinganisha na Kiswahili sanifu yametofautiana. Kwa mfano neno *nka* ambalo ni sawa na neno *nipe* katika lahaja ya Kiswahili sanifu. Kama anavyothibitisha Bakharesa (1992:195) amesema “Lahaja ni tofauti ya matamshi fasaha na matumizi.”

4.19 Matamshi Ya Kimakunduchi Yenye Uvokali/ o, e, u, i, a /

Mtafiti amebaini sauti zinazopatikana katika lahaja ya Kimakunduchi, kama ifuatavyo:

a) Sauti /o/,/e/ hutoa neno botoa na botea.

Katika neno botoa inabeba maana ya kuvunja kama dafu katika lahaja ya Kimakunduchi lakini katika Kiswahili sanifu neno hilo halipo. Pia neno botea ina maana ya mmea unaoota zaidi ya mwaka mmoja. Katika data za utafiti huu mtafiti amegundua jozi bainifu katika neno botoa na kupata ubadilikaji wa irabu kati /o/ na kutolewa irabu /e/.

b)Sauti /a/ imetoa neno kola yenye maana ya chuma (Kimakunduchi),neno hilo hilo linaleta kikwazo katika lahaja sanifu ambapo neno kola hujulikana kama aina ya ukosi hasa kwa nguo za kike.

Katika kuthibitisha sauti hizo zenye uvokali katika lahaja ya Kimakunduchi kwa kuangalia eneo la ulimi ambalo sauti zenye uvokali hutolewa.

Hapa katika data alizopata mtafiti amegundua mgawano wa kimtoano umechukua nafasi, umetokea katikakati ya neno ambapo huleta tofauti katika mazingira ya utokeaji wake katika neno (bo-to-a) tumepata (bo-te-a).

Umbo la ndani

Umbo la nje

Mgawano na Kimtoano


botoa

botea

/ o / → / e /

Kwa hivyo irabu /o/ na /e/ imepata mgawano na Kimtoano.

Kielelezo Na 4.1: Eneo ambalo sauti zenye uvokali hutolewa



Chanzo; Massamba na wenzake, (2004: 39)

Katika jadweli Na (5.8) na kielelezo Na(1) yamebainisha sauti za lahaja ya Kimakunduchi. Katika jadweli Na (5.8) mtafiti amegundua mambo mawili. Moja mahali ambapo sauti zenye ukonsonanti hutokea, na jinsi zinavyotamkwa. Sauti hizo hutamkwa kwenye midomo, midomo na meno, ufizi na meno, kwenye kaakaagumu, kwenye kaaka laini, na pia katika glota.

Kwa upande wa vokali, kielelezo na (1) limebainisha maeneo ya utokeaji wa sauti hizo. Sauti inayotolewa mbele ya ulimi /u/, sauti nyengine hutolewa sehemu ya katika eneo la juu (i), nyengine hutokea nyuma ya ulimi, na nyengine ni sauti /a/ inayotolewa chini ya ulimi.

Katika kipengele hiki cha matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi ambayo huleta vikwazo vya mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na

Kiswahili sanifu kwa kuangalia maumbo ya maneno ya Kimakunduchi yamechunguzwa kutoka umbile lake la asili na hata jinsi maneno hayo yamejitosheleza kimaana ambayo yameleta sitofahamu baina ya makundi hayo mawili. Kutokana na uchunguzi huo kutoka uwandani mtafiti amegundua kuwa watumiaji wa Kimakunduchi wanapokutana peke yao huzungumza kwa kutumia lafudhi yao, lakini wanapokutana na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu hutumia lahaja sanifu. Pia mtafiti anahofia kwa lahaja hii kupotea kwa sababu haina matumizi mapana na haizungumzwi hasa katika shughuli rasmi.

4.20 Matamshi Kubadilika umbo

Lahaja ya Kimakunduchi katika matamshi yake yana tabia ya kubadilika kwa umbo la asili kwa mfano Katika jadweli lifuatalo ambalo linaonesha misamiati ambayo imeundwa kwa kutumia alfabeti zinazojenga maneno kwa lahaja ya Kimakunduchi.

Jedwali Na 4.21: Kubadilika umbo katika Matamshi

Kiswahili Sanifu	Kimakunduchi
Barabara	Barasite
Herini	Herine
winga	Inga
Tafuna	tahuna
Nywili	Nywele
Kologa	Koroga

Chanzo: Data za Uwandani, 2016.

Katika jadweli 4.22 linaonesha kanuni ya ubadilikaji wa umbo la msamiati na kuonesha utofauti wa kimatamshi haileti tofauti ya maana.

Mtafiti amegundua mpishano huru katika msamiati unaonekana katika jadweli kama ifuatavyo:

Maneno	Fonimu zinazopishana
Barabara: Barasite	/ si / na / te /
Herini : Herine	/ i / na / e /.
Inga : Winga	/ i / na / w /.
Tafuna : Tahuna	/ f / na / h /.
Nywele : Nywili	/ e / na / i /.

Data hizi zimemsaidia mtafiti kupata usahihi katika lengo la kuu la utafiti huu lililomtaka mtafiti kuchunguza athari za Kimakunduchi katika Kiswahili ,amegundua mpishano huru hudokeza maana ya *wewe ondoka na mimi niingie*.

Kwa hivyo , fonimu mbili husemekana kuwa katika mpishano huru iwapo zitabadilishana nafasi ya utokeaji na maana isibadilike.

4.20.1 Tofauti Katika Matamshi ya Mazungumzo ya kawaida

Matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi yameathiri kwa wazungumzaji wa Kimakunduchi ambao hutofautiana na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu,kwa mujibu wa msamiati wanaoutumia.

Tuangalie usemaji wao wa kawaida

Kimakunduchi: Nyimbo
Mwanangu Kinole wee *ufugue* macho *ulole*,
Maji yakajaa yanakuja *Unyweleunywele*,
Yakaja juu hulusha *umbi* na ukulele,
Baba *kachinji* kuku Mama *kanletee* mchele,
Unonjo uganga ne wanangu mh! mh!mh!

Kiswahili Sanifu

Mwanangu Kinole fungu macho uone,
Maji yakijaa yanakuja polepole,

Yakafika juu hurusha udongo (vumbi) na ukulele,
Baba amenichinja kuku mama ameleta mchele,
Huu ndio uganga nyinyi wanangu mh!mh!mh!.

Katika nyimbo ya hapo juu, mtafiti amebaini kuwa matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi yameathiri Kiswahili sanifu hata katika mazungumzo ya kawaida. Imebainika kuwa baadhi ya misamiati imepata athari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jedwali Na 4.22: Tofauti katika Matamshi ya Mazungumzo ya Kawaida

KISWAHILI SANIFU	KIMAKUNDUCHI
Uone	Uole
Polepole	Unyweleunywele
Yakafika	Yakaja
Kanletee	Ameleta
Vumbi	Umbi
Amechinja	Kachinji
Huu ndio	Unonjo
Fungua	Ufugue

Chanzo: Data za Uwandani, 2016.

Katika jadweli 4.23 linaonesha tofauti katika matamshi ya mazungumzo ya kawaida ambayo yameonesha mpishano huru kama vile:

Maneno

Fonimu zinazopishana

Uone	:	Uole	/ l / na / n /.
Yakafika	:	Yakaja	/ fi / , / ka / na / ja /.
Vumbi	:	Umbi	/ v /
Fungua	:	Ufugue	/ u / , / n / a , e /.

Katika msamiati umepata uhulutishaji kutoka neno (huu na ndio) → Unonjo.

Katika msamiati *amechinja* amepata kanuni ya udondoshaji katika silabi, hali hii hupelekea kuathiri sauti nyingine na kupata neno *kachinji* ambalo limebadilisha umbo la asili.

Data hizi zilimsaidia mtafiti kufikia lengo mahususi la kutofautisha msamiati wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu unaotumika katika mazungumzo ya kila siku. Data zilizokusanywa na mtafiti amegundua zaidi, athari za matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi baada ya kuona misamiati inayotumika kwa ajili ya mawasiliano baina ya wazungumzaji wa Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ina tofautiana kwa kuangalia sauti zinazotumika katika makundi hayo mawili.

4.20.2 Matamshi ya Sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho /l/

Watafitiwa walitoa misamiati tofauti, lakini mtafitiwa amegundua kuwa baadhi ya misamiati imeathirika kwa kubadilika kwa irabu /u/kuwa kipasuo /d/ au /u/ katika Kiswahili sanifu. Kwa mfano ufuatao:

Jedwali Na 4.23: Matamshi ya Sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho /l/

Matamshi Ya Kimakunduchi	Matamshi Ya Kiswahili Sanifu
1-Muomo	Mdomo
2-Muango	Mlango
3-Kilevu	Kidevu

Chanzo: Data za Uwandani, 2016.

Katika jadwali 4.24 linaonesha athari ya matamshi ya sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho. Msamiati wa neno/ **muomo**/ na/ **muango** / umetumia irabu/ u/ katika Kimakunduchi na kupata badiliko kwa kuingu kwa sauti /d/ na /l/ katika Kiswahili sanifu na kuwa na neno mlango na mdomo. Pia matamshi ya sauti /d/ katika

ubadilikaji wa kilainisho /l/ Kwa mfano wa neno kilevu(Kimakunduchi) na kidevu (Kiswahili sanifu).

Data hizi zilimsaidia mtafiti kutoka kwa walimu 20, wanafunzi 20 ambao walipatikana eneo la Kusini na Kaskazini Makunduchi, aligundua athari kwa kufafanua msamiati ulioimarika kwa konsonanti .Sauti za Kiswahili huimarika na hutokea pale ambapo alofoni za sauti fulani hutamkwa kwa nguvu na ala sauti kuliko wakati wa kutoa sauti yenyewe, badiliko hili huwa la kimazingira, na uimarikaji katika Kiswahili hukumba sauti za likwidi kama kitambaza / l /.

Kwa mfano kutoka katika jadweli linavyoonekana:

1 /l/ → [d] / / n/.

2 Hapa irabu ya / u / hubadilika na kuwa konsonanti ya kipasuo [d] katika mazingira ya kufuatia nazali /n/ mfano, (muomo- mlomo).na hata katika neno muango na mlango irabu ya / u / hubadilika na kuwa konsonati ya kitambaza / l / katika mazingira ya kufuatiwa na nazali / m /.

Tuangalie katika kanuni ifuatayo:

/ u / → [l] /- / m.

4.20.2.1 Matamshi ya Sauti /kana/ badala ya /ana/:

Mtafiti amebaini kuwa lahaja ya Kimakunduchi hutumia sauti [kana], badala ya [ana] katika Kiswahili sanifu, kwa baadhi ya vitenzi vya makundi hayo mawili.vKwa mfano ufuatao:

Jedwali Na 4.24: Matamshi ya Sauti /kana/ badala ya /ana/:

Matamshi ya Kimakunduchi	Matamshi ya Kiswahili sanifu
1- Kan achaka	An ataka
2- Kan acheza	An acheza
3- Kan avita	An apita
4- Kan akwenenda	An akwenda
5- Kan akwimba	An aimba
6- Kan adeka	An adeka
7- Kan alia	An alia

Chanzo : Data za uwandani,2016.

Katika mifano ya msamiati ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu iliyotolewa na wazee 20,vijana 10,walimu 20 wanafunzi 20 ambao wamemsaidia mtafiti kupata data sahihi na amegundua misamiati iliyoonesha katika jadweli 4.25 liaonesha kanuni ya uingizaji neno /kana / badala ya / ana/.

Umbo la ndani	Umbo la nje	Fonimu iliyodhoofika
Kana chaka	Anataka	/k/ na /tʃ/
Kana cheza	Ana cheza	/ k/
Kana vita	Anapita	/ p /, na / v /.
Kanakwenenda	Anakwenda	/ k /, /n/ na //e /
Kanakwimba	Anaimba	/ k/, / w/.
Kanadeka	Anadeka	/ k/.
Kanalia	Analia	/ k/.

Kutokana na mifano iliyopo hapo juu fonimu /k / imebadilika na kuwa kizuiwa kwamiza / tʃ /.

Sauti / p / imedhoofika na kuwa /v/ katika lahaja ya Kimakunduchi.Kwa hivyo kutokana na data zilizopatikana fonimu /k / na kuwa kizuiwa kwamizi /tʃ / katika utamkaji kipasuo /k/ huhitaji nguvu nyingi katika utamkaji ikilinganishwa kizuiwa kwamizwa/tʃ/. Kwa hivyo /k/ imedhoofika.

4.20.2.2 Matamshi ya Sauti /cha/ badala ya /ta/:

Lahaja ya Kimakunduchi ina sauti ya/ cha/ badala ya /ta/ katika Kiswahili sanifu,kwa baadhi ya vitenzi vinavyoonesha wakati ujao na baadhi ya vitenzi huonesha hali ya ukanushi, hivyo hupelekea athari kwa wazungumzaji wa Kiswahili kutokufahamu njeo (wakati) unaotumika katika lahaja ya Kimakunduchi.Tuangalie mifano ya vitenzi vinavyoonesha njeo na hali za sentensi katika jadweli lifuatalo:

Jedwali Na 25: Matamshi ya Sauti /cha/ badala ya /ta/

Lahaja ya Kimakunduchi	Kiswahili sanifu
Kachakuja	Atakuja
Kachakwenda	Atakwenda
Kachachaka	Atataka
Uchachachuka	Utachachuka
Kachabonyeza	Atabonyeza

Chanzo:Data za uwandani,2016.

Katika jadweli la 26, linaonesha athari za matamshi ya sauti / cha/ badala ya /ta/ ambayo yanaonesha madiliko ya kifonetiki ambapo katika utamkaji wa kipasuo kwamiza hubadilika katika mazingira kuingizwa kipasuo si ghuna hubadili umbo kwa kufuatiliwa na konsonati: Kama misamiati ilivyoainishwa katika jadweli la hapo juu.

/tʃ/ → / t/ -/ k/ . Mtafiti alizitumia data hizi alizokusanya kwa wazee 20 kutoka eneo la Kaskazini na Kusini Makunduchi.

4.20.2.3 Msamiati Inayowiana na Inayotofautiana kati ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu

Uchambuzi wa data zifuatazo unalijibu swali lilowataka watafitiwa kubainisha msamiati inayowiana kati ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi ambayo inayopatikana katika sherehe za kimila/kiutamaduni, kielimu na shughuli za kijamii.

Lengo la tatu la utafiti huu ni kubainisha msamiati inayowiana na inayo tofautiana baina ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu, miongoni mwa sababu kuu inayokwamiza mawasiliano kwa wazungumzaji hao ni kutofautiana kwa msamiati Hivyo hupelekekea kutokufahamiana baina ya makundi hayo mawili ambapo kila kundi lina msamiati wake kulingana na muktadha husika. Kuna misamiati inayotumika katika shughuli za kielimu, shughuli za kiutamaduni na shughuli zote zinazofanywa ndani ya jamii.

Jedwali Na 4.26: Misamiati Inayowiana Baina ya Kiswahili Sanifu na Lahaja ya Kimakunduchi

Misamiati ya Kimakunduchi	Misamiati ya Kiswahili Sanifu
Darasa	Darasa
Kulima	Kulima
Kupanda	Kupanda
Embe	Embe
Chungwa	Chungwa
Harusi	Harusi
Kalamu	Kalamu
Moja	Moja
Mbili	Mbili
Tatu	Tatu
Udi	Udi
Mkono	Mkono
Kichwa	Kichwa
Kofia	Kofia
Shati	Shati
Suruali	Suruali
Panga	Panga
Jembe	Jembe
Mahari	Mahari

Chanzo: Data za Uwandani, 2016.

Jadweli Na 4.27 linaonesha orodha ya misamiati inayowiana katika shughuli za kielimu, kiutamaduni na shughuli za kijamii. Misamiati inayotokana katika majina ya matunda, nambari, siku za wiki, viungo vya mwili na misamiati mengineyo.

Data hizi zimekusanywa kutoka kwa watafitiwa huko Makunduchi ambapo zimeweza kujibu dodoso la utafiti huu kwa kubainisha misamiati inayowiana kwa kuzingatia shughuli mbalimbali za kijamii.

Mtafiti ameweza kubainisha misamiati hiyo kama inavyoonekana katika jadweli lilotangulia:

- i) Misamiati iliyapatikana katika shughuli za kielimu:
Kalamu, darasa, moja, mbili, tatu.(nambari).
- ii) Misamiati iliyopatikana katika shughuli za kiutamaduni:
Mahari, harusi, udi, kofia.
- iii) Misamiati inayopatikana katika shughuli za kijamii:
Kulima, panga, jembe, shati, suruali, kichwa, mkono.

Katika uchambuzi wa data hizi ,mtafiti amebaini kuwa wazee wamebainisha msamiati hasa katika shughuli za kiutamaduni na kijamii kwa asilimia 75%, walimu na wanafunzi wametoa misamiati ya kielimu na kijamii kwa asilimia 55% ,na vijana wametoa misamiati ya kijamii kwa asilimia 35%.Data hizi zimekusanywa kwa njia ya mahojiano na hojaji.

Katika uchambuzi wa data zifuatazo umelijibu katika dodoso zake kuwa kuna misamiati kadhaa ambayo imetofautiana baina ya Kiswahili sanifu na

Kimakunduchi. Watafitiwa wamebainisha misamiati hiyo inayotokana na lahaja ya Kimakunduchi.

Jedwali Na 4.27: Kubainisha Msamiati Inayotokana na Lahaja ya Kimakunduchi

Misamiati ya Kimakunduchi	Misamiati ya Kiswahili Sanifu
Kipangaa	Kifuu
Umeta	Umeme
Haha	Njaa
Kunuto	Chujio
Mzi	Uzi
Mvyazi	Mzazi
Mwanakele	Mtoto
Gogota	Kohoa
Chimwene	Askari
Kimandaa	Kioo
Mshenga	Mposaji
Sufuria	Dishi
Ua	Ukuta
Kukeza	Kunyonyesha
Kukaza	Kupendezwa
Nguo	Kanga
Kinumbi	Kikapu
Kuwangasa	Kuwasusa
Kuolegwa	Kuolewa
Nyambo	Pweza
Kimombo	Kiingereza
Mkindwi	Uporo
Kuvyeze	Kuamka

Chanzo; Data za Uwandani,(2016)

4.20.2.4 Kubainisha Utamkaji wa asili na Utamkaji wa Sasa

Matokeo ya utafiti huu umekusanya misamiati ambayo inabainisha utamkaji wa asili na utamkaji wa sasa katika lahaja ya Kimakunduchi.

Jedwali Na4.28: Kubainisha Utamkaji wa Asili na Utamkaji Wa Sasa

Utamkaji wa Asili	Utamkaji wa Sasa
Shomoo	Chomoa
Limbika	Fungo
Kuwinja	Kusaka
Makoa	Magomba
Koka	Kunyonya
Wavyale	Wazaliwa
Kunguto	Chujio
Kale	Zamani
Kimamo	Chombo
Sopo	Kopo/kata
Pocho	Bovu
Vihaba	Vichache
Usoni	Mbele
Ngema	Nzima
Kipangaa	Kifuu
Afiki	Rafiki
Mwiku	Uporo
Mitingi	Kitini
Mabwe	Mawe
Tanu	Mkungu
Kazu	Nguo
Nguo	Kanga
Kinumbi	Kikapu
Mwana	Mtoto
Nyambo	Pweza
Fya	Jiko
Ndo	Ndio
Njoga	Njoo
Guyu	Guu
Umeta	Umeme

Chanzo: Data za Uwandani (2016).

Data hizi zimepatikana kwa njia ya mahojiano, na dodoso kama inavyojidhihirisha hapo juu. Mtafiti amebainisha msamiati kwa asilimia (45%) watafitiwa wanatamka katika utamkaji wa asili, na utamkaji wa sasa kwa asilimia (60%). Matokeo haya yanamaanisha kuwa lahaja ya Kimakunduchi msamiati wa asili imepotea ambapo wazaliwa wa sasa hawajui. Pia imepata athari ya ubadilikaji wa umbo.

4.20.2.5 Maoni ya Watafitiwa Jinsi ya Kupunguza Athari za Kimakunduchi Katika Kiswahili Sanifu

Data zifuatazo zinaonesha maoni juu ya kuondosha athari za Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu na zimechambuliwa kwa kutumia nadharia ya muachano na makutano ya Byrni 1980. Nadharia ya muachano inafafanua jinsi wazungumzaji wanavyoiacha lahaja mama na kutumia lahaja nyingine katika mawasiliano na ile ya makutano inafafanua wazungumzaji wa lahaja moja wanapokutana katika mawasiliano hujenga mafahamiano katika mazungumzo yao. Jaduweli lifuatalo hapo chini linabainisha data hizo.

Jedwali Na 4.29: Maoni Juu ya Kupunguza Athari za Kimakunduchi Katika Kiswahili Sanifu

Nambari	Hoja	Waliokubali (idadi na asilimia)	Waliokanusha	Jumla	Maoni ya mtafiti
		idadi na silimia)	(idadi na asilimia)	(idadi na asilimia)	
1	Kutolewa kwa elimu inayohusu umuhimu wa lahaja katika sehemu fulani.	(40)50%	(40)50%	(80) 100%	
2	Kuwe na vipindi maalumu katika vyombo vya habari vyenye kuelezea juu ya lahaja ya Kimakunduchi.	(36)45%	(44) 55%	(80) 100%	
3	Lahaja itumike mashuleni kulingana na eneo lake.	(48) 60%	(32) 40%	(80)100%	
4	Kuwekwa kwa tamasha la asili ambalo huonesha vyakula vya asili,vya kiutamaduni.	(35) 45%	(45) 55%	(80) 100%	
5	Kutoruhusu kuingia wageni kiholela.	(44) 55%	(36) 45%	(80) 100%	
6	Kutumika sarufi moja baina ya lahaja hizo.	(35)54%	(45) 56%	(80) 100%	
7	Kuwepo kwa kumbukumbu za kutosha katika maktaba zetu zinazohusu Kimakunduchi.	(28) 35%	(52) 65%	(80) 100%	

Chanzo: Data za Uwandani (2016).

Katika jadwali 4.30 linaonesha maoni juu ya kupunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu kutoka kwa watafitiwa 80, wazee 20, vijana 20, walimu 20 na wanafunzi 20, waliopo eneo la Kaskazini na eneo la Kusini Makunduchi. Mtafiti amegundua maoni hayo ilisaidia kupunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi, ijapokuwa wapo waliokubali kwa asilimia na waliokataa katika hoja hizo.

4.20.2.6 Kutolewa Elimu ya Lahaja

Data zinaonesha kuwa watafitiwa waliokubali na waliokataa asilimia sawa sawa (50%) kutoka eneo la kaskazini na kusini Makunduchi, kuhusu kutolewa kwa elimu inayohusu umuhimu wa lahaja katika sehemu fulani. Uchambuzi huu umefanywa kwa kutumia nadhari ya makutano ambapo watafitiwa wanaozungumza lahaja moja wanakubaliana na kufahamiana katika mawasiliano ndio maana ikajitokeza asilimia sawa.

4.21 Kuwekwa Vipindi Maalum Katika Vyombo Vya Habari

Watafitiwa wametoa mapendekezo yao, katika kuondoa athari katika lahaja ya Kimakunduchi, vyombo vya habari vya Serikali au vyombo vya habari binafsi wachukue nafasi ya kuunda vipindi vinavyoitangaza lahaja ya Kimakunduchi ili watumiaji wa lahaja sanifu waielewe vizuri katika matamshi yake. Data zinaonesha kuwa watafitiwa waliokubali wana asilimia (36%) na waliokataa wana asilimia (44%) kutoka eneo la Kaskazini na Kusini Makunduchi, kuwekwa kwa vipindi maalumu katika vyombo vya habari. Uchambuzi wa utafiti huu umefanyika kwa kupitia nadharia ya muachano ambapo watafitiwa wanaozungumza lahaja ya

Kimakunduchi na lahaja sanifu wameachana na hata asilimia zao zimetafautiana kama matokeo katika jadweli Na (6.7). Mtafiti amependekeza kwa watafitiwa kutokuachana na wasitafautiane katika mitazamo yao,wawe na mitazamo sawa. .Lengo la utafiti huu ni kuondoa athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

4.22 Lahaja Itumike Mashuleni

Mtafiti amekusanya matokeo katika jadweli Na (6.7), yameonesha kuwa asilimia (48%) ya watafitiwa wamekubali, na watafitiwa asilimia (32%) wamekataa. Kutokana na matokeo ya watafitiwa asilimia 48% kukubali inadhihirisha kuwa watafitiwa wameikubali kwa kiwango kikubwa sana, mchambuzi ametumia nadharia ya Makutano ambapo lengo la mtafiti ni kuikutanisha jamii ya Wamakunduchi asilia na watakaozaliwa kwa kurithishana kwa kupitia sekta muhimu ya elimu.Kufanya hivyo kutapelekea kuwepo kwa athari nzuri ya urithi baina ya wazungumzaji wazawa wa lahaja ya Kimakunduchi na wazungumzaji wa Kiswahili sanifu kuitumia lahaja hiyo kwa mawanda mapana.

4.23 Kuwekwa Kwa Tamasha La Utamaduni Asilia

Data zinaonesha kuwa watafiwa wa Kaskazini na Kusini Makunduchi kwa asilimia (35%) wamekubali kuwekwa kwa tamasha la utamaduni ambalo litaonesha vitu asilia ,kama mavazi na vyakula, na asilimia(45%) ya watafitiwa wamekataa kuwekwa tamasha.Kutokana na uchambuzi uliofanywa na mtafiti na kutumia nadharia ya Makutano ambayo hukutanisha watu tofauti waliowazawa na wasiokuwa wazawa kutoka sehemu tofauti watapata misamiati tofauti ambayo

yatapatikana katika vitu asilia katika tamasha hilo.Kwa watafitiwa waliokataa hawafahamu lengo la mtafiti.Kwa hivyo kuwekwa kwa tamasha kutapelekea kuitangaza lahaja ya Kimakunduchi na litaweka kumbukumbu katika shughuli walizokuwa wakifanya wazee hapo kale.

4.24 Kutoruhusu Kuingia Kwa Wageni Kiholela

Katika jadweli namba(6.7) linaonesha kuwa asilimia (44%) ya walengwa wote walieleza miongoni mwa sababu kuu inayoipata lahaja ya Kimakunduchi ni uingiaji wa wageni kiholela katika kijiji cha Makunduchi,watafitiwa asilimia(36 %) wamekataa kwamba wageni waruhusiwe . Uchambuzi wa utafiti huu umefanyika kwa kutumia nadharia Muachano ambayo hupelekea mwingiliano mkubwa na kuacha athari hasa kwa vijana kuiga lugha za wageni hao na kusahau lahaja yao iwe kwa kuiga au kwa njia yoyote ile.Huingiza misamiati yao ambayo haiendani na lahaja ya Makunduchi hatimae kuiharibu na kuleta vikwazo katika mawasiliano baina ya(wenyeji) wazawa na wageni kwa Makunduchi.Kwa hivyo kutokana na asilimia kubwa waliokubali kwamba wageni wasiruhusiwe kiholela nakubaliana nao , si busara kuingiza wageni kiholela ambao huacha athari mbaya katika jamii tuwe macho katika hili.

4.25 Kutumika Kwa Sarufi Moja

Katika uchambuzi wa data,mtafiti amebaini kuwa watafitiwa wote kwa asilimia(35%) wamekubali hoja ya kutumika kwa sarufi moja yenye kufanana katika maumbo ya maneno,matamshi na hata matumizi ya maneno hayo kufanana. Na watafitiwa kwa asilimia 45% wamekataa hoja hii.Uchambuzi wa data hizi

umefafanunuliwa kwa kutumia nadharia ya makutano ambayo huwaunganisha watu wanaozungumza lugha zenye kufanana sarufi zao ambazo hazileti vikwamizi katika mawasiliano. Nakubaliana na waliokubali hata kama wamepata asilimia ndogo. Hali hii ikifuatwa itaondoa athari baina ya Lahaja mbili, kati ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu.

4.26 Kuwepo Kwa Kumbukumbu Za Kutosha

Mtafiti amekusanya data na kupata matokeo ya utafiti huu yamepatikana kwa asilimia (28%) wamekubali na asilimia (52%) wamekataa kama inavyoonekana katika jadweli Namba(6.7). Uchambuzi wa utafiti huu umefanywa kwa kutumia nadharia ya makutano ambapo husaidia kukutana kwa wasomi, wakufunzi wa lugha ya Kiswahili hasa lahaja ya Kimakunduchi kupata marejeleo katika uandishi wa kazi zao. Nakubaliana na watafiti wote waliokubali inaonekana wana muamko katika taaluma hata kama jadweli linaonesha wapo kwa asilimia ndogo. Pia nashauri kwa maktaba zote zilizomo nchini kuwekwa kumbukumbu za kutosha ikiwemo vitabu, vijarida, vipeperushi na hata tasnifu zinazohusu lahaja ya Kimakunduchi. Kufanya hivyo kutasaidia kuwaathiri wasomi kuifuatilia lahaja hii kwa kuiandikia kazi maalumu na kufanya marejeleo ya tasnifu kazi nyengine.

4.27 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika sura hii mtafiti amewasilisha na kufafanua taarifa za kiisimu jamii za watafiti waliokusudiwa katika utafiti huu. Mtafiti amebainisha wazi na kufafanua vipengele vya matamshi vya lahaja ya Kimakunduchi. Pia mtafiti amebainisha na

kufafanua athari za matamshi katika lahaja ya Kimakunduchi na kuainisha mapendekezo ya kuondoa athari hizo.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa watafitiwa katika kundi la wazee ndio wanaotumia misamiati inayotofautiana katika lahaja ya Kimakunduchi kwani ndio yenye asili ya Kimakunduchi , vijana ,walimu na wanafunzi ndio wanaotumia misamiati inayolingana baina ya Kiswahili sanifu na Kimakunduchi kwa sababu hutumia katika mazungumzo yao ya kawaida ukilinganisha na wazee.Halikadhalika mtafiti aliwataka watafiti kubainisha misamiati iliyopatikana na kuanisha utamkaji wa asili na utamkaji wa sasa.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho la utafiti wa lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathiriwa katika Kiswahili Sanifu, Lengo kuu katika sura hii ni kuonyesha matokeo muhimu ya utafiti huu. Sura hii imegawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza, inahusu muhtasari wa utafiti kwa ujumla. Sehemu ya pili, inaelezea matokeo ya Utafiti. Sehemu ya tatu, inaelezea mapendekezo juu ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhutajari kuhusu Utafiti

Utafiti huu wa lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathiriwa katika Kiswahili sanifu. Utafiti huu ulilenga kuchunguza athari juu ya msamiati ambayo hukwamiza mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na lahaja sanifu. Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu, lengo la kwanza, kubainisha msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi. Lengo la pili, kufafanua athari za lahaja ya Kimakunduchi katika mazungumzo ya Kiswahili sanifu. Lengo la tatu kueleza tofauti baina ya msamiati unaowiana baina ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi. Umuhimu wa kufanya ufafanuzi huu wa lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathiriwa katika Kiswahili sanifu ni kuongeza maarifa mapya kwa taaluma ya isimu. Pia, umewasaidia wahadhiri, wanafunzi wa vyuo vikuu kutumia kama ni marejeleo katika tasnifu zao. Hata hivyo, kwa wasomaji wengine wasiokijua Kimakunduchi kuvielewa vipengele vya matamshi vya Kimakunduchi vinavyotumika katika Kiswahili sanifu

kwa lengo la kufanikisha mawasiliano baina ya mzungumzaji na msikilizaji wake (hadhira na fanani).

Utafiti huu ulifanyika Makunduchi katika wilaya ya kusini Unguja na ulihusisha eneo la Kaskazini na eneo la Kusini ikiwemo Kajengwa, Mtongani, Tasani, Kae kuu na Sokoni na kuteua skuli ya Kusini na Skuli ya Makunduchi ambayo ni kuu hapo Makunduchi. Maeneo haya yaliyoteuliwa kwa sababu wazee wa zamani wapo ndio walengwa wakuu wa utafiti huu. Jumla ya watafitiwa 80 walishirikishwa katika utafiti huu kwa kuzingatia rika(wazee 20, vijana 20, walimu 20, na wanafunzi 20). Uteuzi huo ulifanyika kwa kugawa watafitiwa kwa kila kundi liligaiwa kwa maeneo (Kaskazini na Kusini). Usamplishaji nasibu ulitumika kupata watafitiwa wa utafiti huu kwa kuzingatia vigezo vya umri na jinsia. Lengo lilikuwa kufahamu watumiaji Msamiati ipi katika makundi hayo. Katika ukusanyaji wa data za utafiti huu zilifafanuliwa kwa njia ya kiidadi na kimaelezo.

Mkabala wa kinadharia uliotumika ni Mkabala wa nadharia ya Muachano na Makutano ya Giles na Byrne(1982). Kwa kutumia nadharia hii, watafitiwa wa utafiti huu wanatumia vipengele hivyo katika mazingira yao ya mawasiliano yao ya kila siku. Nadharia hii imeelezea kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi huleta athari wanapofikia hatua ya kuacha lahaja hiyo, katika mawasiliano ya kila siku na kutumia lahaja nyengine yaani (Kiswahili sanifu). Hali hii ikitokea hujulikana kama ni makutano. Pindi akirudi Makunduchi hurejea lahaja yake. Kwa mtizamo huu nadharia ya muachano hapa huchukua nafasi. Kutokana na utafiti huu, mtafiti ameonesha athari zinazofanywa na wazungumzaji hao katika mazungumzo ya

kawaida na kufafanua mapendekezo juu ya athari hizo. Pamoja na hayo athari za matamshi ambazo zilibainishwa na kufafanuliwa kwa kufafanua msamiati inayotumika katika mawasiliano ya kila siku.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu mtafiti aligundua kwa kutumia lengo la kwanza kwa kubainisha msamiati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu, baadhi ya msamiati ambayo imepatikana na mtafiti, amebaini kwa kuuliza suali ambalo mtafiti aliwataka watafitiwa kuandika msamiati inayotumika katika lahaja ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi. Mtafiti amebaini kuwa kuna msamiati inayotumika kwa wazungumzaji wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ambayo hutumika katika mazungumzo ya kawaida ambayo hufanana, Aidha mtafiti katika kulijibu suali hili amebaini, kuna baadhi ya msamiati hukwamisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa makundi hayo mawili na kugawika katika misamiati ya majina ya siku, nyakati, misamiati ya walemavu, misamiati ya majina ya ukoo, misamiati ya kazi ambazo hufanywa na jamii husika.

Kufafanua athari ya lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu: Katika lengo la pili, lilemalo fafanua athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu. Mtafiti amesaidiwa na suali lilemalo “lahaja ya Kimakunduchi imekutwa na athari yoyote? Kama Ndio taja athari hizo”? Mtafiti amebaini kuwa zipo athari hizo zinazokwamisha mawasiliano ikiwemo athari za kiumbo, matamshi, na matumizi ambapo wazungumzaji wa lahaja hizi mbili hupelekea kutoelewana na kutofautiana katika mazungumzo. Kwa kuchunguza msamiati ambayo imebeba athari katika

matamshi, matumizi, maumbo. Aidha mtafiti amebaini kwa kiwango kikubwa athari ambazo zimedhihirishwa katika mtizamo wa matamshi na matumizi ya lahaja hiyo ni pamoja na :

- a) a) Udondoshaji wa kilainisho /l/ na kimadende /r/
- b))Uingizaji wa sauti –y- pamoja na Uingizaji wa sauti –ly-.
- c) Uingizaji wa sauti /nch/, /k/, /j /, na /w/.
- d) Uingizaji wa sauti /v/, na /vy/ katika lahaja ya Kimakunduchi
- e) Matamshi yenye kubadilika umbo (athari katika umbo).
- f) Matamshi yenye uvokali /o/, /ɛ/, /u/, /i/, /a/.
- g) Matamshi ya sauti /d/ na hubadilika irabu /u/ na kilainisho /l/.
- h) Matamshi ya sauti /kana/ badala ya /ana/
- i) Matamshi ya sauti /cha/ badala ya /t/

Katika vipengele hivyo ni vya kifonolojia ambavyo vinatokana na matamshi ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu ndivyo vinavyobainisha athari zinazokwamisha mawasiliano kati ya wazungumzaji wa Kiswahili na lahaja ya Kimakunduchi na kupelekea kutofahamiana katika mazungumzo kati ya mtu na mtu, au eneo moja na jingine.

Kueleza tofauti na uwiano wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu, Katika lengo la tatu, lisemalo kueleza tofauti na uwiano wa lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Mtafiti amesaidiwa na suali lisemalo “Ni kitu gani kinachotofautisha ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu? Katika kujibu suali hili mtafiti amegundua kuwa kuna sababu tofauti ambazo hutofautisha

lahaja,amebaini kuwa kuna sababu....ambazo ni utofauti wa lafudhi, kiimbo, kiumbo na kiwango kikubwa ni tofauti ya matamshi .Aidha katika utafiti huu mtafiti amepata data za uwiano wa msamiati ambapo mtafiti amesaidiwa na suali lisemalo, “Bainisha misamiati inayowiana kati ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu na Kimakunduchi?” Katika kulijibu suali hili mtafiti amegundua kuna msamiati tofauti ambayo imewiana ikiwemo ya makundi ya matunda,nambari, siku,msamiati ya viungo vya mwili.Pia amebaini msamiati kwa makundi ya kijamii yanayotumia zaidi misamiati ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi.Makundi haya ya kijamii ni wazee (20), vijana (20), walimu (20) na wanafunzi (20).

Sababu zinazofanya makundi haya yatumie msamiati hiyo ni kwamba watafitiwa wengi wa makundi haya ni wenye asili ya jamii ya Wamakunduchi na wanaishi vijijini. Kwa hivyo wana umahiri wa kutosha katika uzungumzaji wa Kimakunduchi kuliko Kiswahili sanifu.Pia, watafitiwa wa makundi hayo baadhi yao wanauelewa mdogo wa kutofautisha matamshi kati ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu.Sababu hizi ndizo zinazowafanya watafitiwa hawa watumie matamshi ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu.

Halikadhalika matokeo ya Utafiti huu, misamiati amegundua athari kwa upande wa wanafunzi 20, walimu 20, vijana 20 na wazee 20. Baada ya kufanyiwa utafiti katika msamiati, imegundulikana kuwa kuna tofauti ya matamshi, maumbo ya msamiati, ambayo hukwamiza mawasiliano kwa watumiaji wa lahaja ya Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi.

5.2.1 Mapendekezo Kuhusu Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulijikita katika kufafanua athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili sanifu kwa kuegemea zaidi kwenye msamiati na utamkaji wake katika Wilaya ya Kusini (Makunduchi) na umebainisha vipengele mbalimbali vya matamshi ya Kimakunduchi vinavyotumika katika Kiswahili sanifu ambavyo ni vya kifonolojia.

Mtafiti anapendekeza kufanyike utafiti wa lahaja za Kiunguja mjini, Kimakunduchi kwa kutumia msamiati na utamkaji wake na kuangalia zaidi kipengele cha sintaksia na maana .Kwa lengo la kupata kugundua ukweli alioupata mtafiti kuwa Kimakunduchi kinafanana na kinatofautiana katika lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili Sanifu ,pia kugundua kuwa ukweli wa kuwa ufafanuzi wa athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili Sanifu umegundulikana katika utamkaji wa misamiati au la.

Muhtasari wa Sura

Sura hii iliwasilisha matokeo ya utafiti huu.Imebainisha malengo mahususi na kuyafafanua kwa kujihusisha na nadharia ya Makutano na Muachano ya Byrne na Giles (1982) na kuonesha jinsi ilivyochangia kufikia lengo la jumla la utafiti.Sura hii imeanza na utangulizi, malengo mahususi kwa kuhusisha na nadharia ya makutano na muachano. Aidha imeelezea kwa muhtasari wa matokeo ya utafiti huu pamoja na muundo mzima wa tasnifu.Baadhi ya vipengele vya sura hii ni hitimisho, mapendekezo kwa tafiti za baadaye, kwa lengo la kupunguza pengo kwa liliopo kuhusu marejeo ya lahaja za Kiswahili.

MAREJEO

- Babbie, B. (1999). *The basis of social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bakhresa, S. K. (1992). *Kamusi ya Maana Na Matumizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salam: Longhorn Publisher Ltd.
- BAKIZA, (2012). *Kamusi La Lahaja Ya Kimakunduchi*. Dar es Salaam: Jamana Printers Ltd.
- Chiraghdid, D. na Mnyapala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam: Oxford University Press.
- Chum, H. (1994). *Msamiati wa Pekee wa Kikae*. Stocholm: Nordic Association of African Studies.
- Crystal, D. (2003), *The Cambridge Encnclopedia of Language*, (Toleo la 2), New York, Cambridge University Press.
- Enon, J. C. (1998). *Educational Research Statistics and Measurement*, Kampala: Makerere University Press.
- Juma, A. M. (2011). *Ulinganishaji wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kizimkazi*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Juma, M. A. (2006). *Msamiati Wa Vitenzi Katika Lafudhi za Jambiani, Paje, na Bwejuu Katika Lahaja ya Kimakunduchi*, Tasnifu ndogo ya B.A (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Taifa Cha Zanzibar.
- Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Kombo, D. na Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis writing. An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Method and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited.
- Maganga, C. (1991). *A Study of The Morphology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu, and Kimakunduchi*. Unpublished M.A Kiswahili Dissertation, University of Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, Dar-es-Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. (2012). *Misingi ya Fonolojia*: Dar es Salaam: TATAKI.
- Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*, Nairobi: Longman (K) Limited.
- Mohammed, S. (1984). *Urban Versus Rural Swahili (A study of Pemba Varieties)* Zanzibar, Haijachapishwa. *Swahili and Sabaki A Linguistic History*.
- Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu jamii Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: TUKI.
- Polome, E. (1980). *Language, Society and Poleo culture*. Stanford: Stanford University Press.
- TATAKI, (2014), *Kioo Cha Lugha*, Chuo Kikuu cha Dares Salaam, Tanzania.
- Whitely, W. (1969). *Swahili. The Rise of a National Language Lower*. Brydon: Great Britain.

VIAMBATANISHO

KIAMBATISHO NAMBA 1: KIONGOZI CHA MAHOJIANO

Maswali ya Utafiti ya Wazee

1. (a) Una umri gani? -----
 (b) Unafanya kazi gani? -----
 (c) Kiwango chako cha elimu ni kipi? -----
 (d) Lugha yako ya kwanza ni ipi? -----
2. (a) Umezaliwa wapi? -----
 (b) Umeishi muda gani? -----
3. Nitajie msamiati ifuatayo inayotumika katika lahaja ya Kimakunduchi, Kama vile ugali, nywele, moshi, tafuna, tikisa, chutama, koroga, inga, chungu, na jicho.
4. Je, wewe mwenyewe hutamka msamiati huo? Kama ndiyo taja msamiati mengine unayoyafahamu tofauti na hayo yaliyotajwa katika swali la 3.
5. Kwa maoni yako, je, unafikiri ni makundi gani kijamii hupendelea kutumia matamshi ya lugha ya Kimakunduchi katika Kiswahili cha mazungumzo?
6. Je, wewe mwenyewe unafikiri lahaja ya Kimakunduchi imekutwa na athari
7. Je, kwa maoni yako, unafikiri nini kifanyike kupunguza athari za lahaja ya Kimakunduchi katika Kiswahili?

Asante kwa ushirikiano wako.

MISAMIATI YA MAPAMBO,MILA NA UTAMADUNI

Kimakunduchi	Kiswahili sanifu

MISAMIATI YA WATU WENYE ULEMAVU

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU

MISAMIATI YA MALIPO

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU

10. Bainisha misamiati inayowiana na inayotofautiana baina ya Kiswahili sanifu na Lahaja ya Kimakunduchi.

MISAMIATI INAYOWIANA

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU

MISAMIATI INAYOTOFAUTIANA

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU

AHSANTE KWA MSAADA WAKO

8. Kwa maoni yako, unadhani nini kifanyike kuondoa athari hizo kwa,

a) vijana

i)

ii)

iii)

b) wazee

i)

ii)

iii)

c) walimu

i)

ii)

iii)

d) wanafunzi

i)

ii)

iii)

6. Naomba unitajie misamiati isiyopungua (20) inayotumika katika Kiswahili sanifu na Kimakunduchi.

KIMAKUNDUCHI	KISWAHILI SANIFU

7. Kuna tofauti ya matamshi baina ya misamiati ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu?kama ndiyo ni misamiati ipi ina utofauti wa matamshi kati ya lahaja hizo.

.....
.....
.....

7b) Kuna misamiati yoyote inayofanana baina ya lahaja ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu? Kama ipo, naomba unibainishie ,

.....
.....

8. Lahaja ya Kimakunduchi imekumbwa na athari yoyote kwa wazungumzaji ya sasa?

.....
.....

9. Kuna vikwazo vyovyote vinavyokwamisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa kale na wa sasa katika Kiswahili sanifu na lahaja ya Kimakunduchi?

.....

.....

.....

10) Kwa maoni yako nini kifanyike kuondoa athari hizo kwa ,

Wazee.....

.....

.....

Vijana.....

.....

.....

.....

Walimu.....

.....

.....

Wanafunzi.....

.....

.....